SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.24 NO. 2 2025
DOI: 10.51984/JOHS.V24I2.4399

جامعة سبها للعلوم الإنسانية مجلة
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: http://www.sebhau.edu.ly/journal/johs

MATUMIZI YA KIAMBISHI " H-" KATIKA MIKTADHA MAALUMU YA KIISIMU YA KISWAHILI

Taher Mohammed Amhammed Mohammed Ali

Department of African Languages and Studies, Faculty of Languages, Sebha University, Libya

Keywords:
kiambishi " h-" mofimu
Kiswahili
Isimu
Viambishi
Matumizi

IKISIRI

Utafiti huu unahusu matumizi ya kiambishi " h-" ambacho kina kazi maarufu katika sarufi ya Kiswahili hasa katika kuonesha ukanushi. Lakini katika utafiti huu kiambishi hiki kina matumizi anuwai katika lugha. Kutambua kazi kutambua kazi ya kisarufi ni taaluma ya lugha (Isimu). Kiambishi hiki pia hutokea katika matumizi ambayo si ya kiisimu. Utafiti huu ulifanyika mjini Zanzibar kwa watafitiwa wanaotumia Kiswahili katika shughuli zao. Mbinu na zana zilizotumika zilihusu kudurusu makala katika maktaba, hojaji, na mahojiano kwa watafitiwa. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba watumiaji wa lugha, hata kama si wanaisimu, lakini wanazingatia usahihi wa kanuni za lugha. Aidha taaluma ya isimu ni muhimu katika kufungua njia na kueleza yale wanayoyajua. Kiambishi " h-" kina maumbo mbalimbali, kinafanya kazi kama mofimu na pia katika matumizi ya muundo unaokubaliwa na Kiswahili. Matokeo hayo ya utafiti yanashawishi kwamba kuna haja ya kufanya utafiti mpana zaidi katika lahaja mbalimbali za Kiswahili kwa kuwashirikisha watumiaji wa kawaida wa Kiswahili kwa sababu ujuzi na taaluma vinashirikishana.

استخدام البادئة (H-) في البنية اللغوية في اللغة السواحيلية"

محمدامحمد علي الطاهر

قسم اللغات والدراسات الافريقية، كلية اللغات جامعة سبها ،ليبيا

الكلمات المفتاحية:
البادئة*h*- اللغوية
مورفيم
استخدام
البادئات

الملخص

تتناول هذه الدراسة استخدام اللواحق الصرفية، وبشكل خاص اللَّاحقة "h-"، التي تؤدي وظيفة معروفة في قواعد اللغة السواحيلية، ولا سيما في الدلالة على النفي، غير أنّ نتائج البحث تكشف أن لهذه اللاحقة استخدامات متعدّدة تتجاوز هذا المعنى التقليدي في إطار اللغة، إنَّ التعرّف على الوظائف القواعدية للعناصر اللغوية يُعَدُّ من صميم علم اللغة (اللسانيات)، غير أن هذه اللاحقة تظهر كذلك في استعمالات غير لسانية ذات دلالات متنوّعة، وقد أُجري هذا البحث في مدينة زنجبار، مستهدفاً متحدثي السواحيلية الذين يستخدمونها في أنشطتهم الحياتية والمهنية، اعتمد الباحث على مجموعة من المنهجيات والأدوات البحثية، شملت مراجعة شاملة للمقالات والدراسات في المكتبات، بالإضافة إلى استخدام الاستبيانات والمقابلات مع عينة من المشاركين، وأظهرت نتائج الدراسة أن مستخدمي اللغة - حتى أولئك الذين ليس لديهم خلفية متخصصة في اللسانيات يُبدون وعياً ملحوظاً بصحة القواعد، ويميلون إلى الالتزام بها أثناء تواصلهم، كما تؤكد النتائج أن دراسة علم اللغة تُسهم بشكل أساسي في توضيح البنى القواعدية والكشف عن آليات عملها، مما يفتح آفاقاً لفهم أعمق لبنية اللغة السواحيلية، أوضحت الدراسة كذلك أن اللاحقة "h-" تتخذ أشكالاً متعددة، وتؤدي وظائف صرفية باعتبارها مُورفيماً، فضلاً عن دورها في بناء التراكيب المعتمدة في اللغة السواحيلية. تشير النتائج في مجملها إلى وجود حاجة ملحّة لإجراء المزيد من الأبحاث المتعمقة حول هذه الظاهرة عبر اللهجات المتنوعة للغة السواحيلية، مع إشراك المتحدثين الأصليين في الدراسات الميدانية، نظراً إلى أهمية تلاقي المعرفة النظرية مع الخبرة الاستعمالية في إثراء الفهم اللغوي الشامل.

SURA YA KWANZA
UTANGULIZI

1.0 Utangulizi

Hii ni sura tangulizi ambayo inaeleza kwa muhtasari namna utafiti huu

*Corresponding author:
E-mail addresses: moh.taher@sebhau.edu.ly

Article History : Received 06 September 2025 - Received in revised form 08 November 2025 - Accepted 30 November 2025

ulivyokusudiwa
kufanyika kwa kutaja usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, mawanda ya utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na kufafanua ukomo wa utafiti.

1.1 Usuli wa Mada

Viambishi ni mada mojawapo ambayo baadhi ya wataalamu kama vile Khamis (2011) na Mgullu (2010) huwa waliizungumzia. Ni pande au viangama ambavyo aghalabu huhusishwa na vitenzi na nomino. Viambishi vina kazi mahsusi za kiisimu. Kazi hizo ama zahusu kubainisha hali ya umoja au wingi, au pia hufanya kazi ya kuonesha matumizi yakiwemo matumizi ya nafsi, wakati (njeo) na urejeshi. Baadhi ya wanaisimu kama vile Kihore na wenzake (2012) wameonesha kuwa viambishi ndivyo vitumikavyo katika kuunda maneno pamoja na kupelekea maana mpya.

Kwa kawaida viambishi huwa ni vipande vidogo vidogo vya neno. Vipande hivyo ni lazima vibebe maana ya kisarufi. Mantiki hiyo yafahamisha kuwa siyo kila kipande cha neno huwa ni kiambishi. Masharti ya kiambishi ni utoaji wa maana ya kisarufi au ya kileksika. Kutokana na mitazamo ya wanaisimu yadhihirisha kuwa viambishi vya Kiswahili aghalabu hutokea kabla au/na baada ya mzizi wa neno. Viambishi ambavyo hutokea kabla, mara nyingi ndivyo vyenye kubadili neno kutoka kategoria moja ya maneno na kwenda aina nyingine. Kwa mfano,

1. **Jedwali 1: Viambishi vya kategoria za maneno**

Kabla ya Mabadiliko	**Baada ya Mabadiliko**
Safi (Kielezi/Kivumishi)	**U**safi (Nomino)
Cheza (Kitenzi)	**M**chezo (Nomino)
Zuri (Kivumishi)	**U**zuri (Nomino)
Lima (Kitenzi)	**M**limaji (Nomino)
Vuta (Kitenzi)	**M**vuto (Nomino)

Katika **Jedwali 1** hapo juu vile viambishi vinavyotokea kabla na baada ya mzizi ndivyo ambavyo hubadilisha neno katika kategoria mpya.

2. Pia viambishi hubadilisha kauli ya Kitenzi kama katika Jedwali lifuatalo
3. **Jedwali. 2**: Viambishi na mabadiliko ya msamiati

	Vitenzi kabla ya mabadiliko ya kauli	Vitenzi baada ya Mabailiko ya kauli
(i)	Piga	Pig**w**a, pig**ik**a, pig**an**a
(ii)	Imba	Imb**w**a, imb**ik**a, imb**ia,** imbi**an**a,imbi**an-eni**
(iii)	Kera	Ker**w**a, ker**ek**a, ker**an-en**i, ker-**eh-esh**a

Katika **Jedwali 2** hapo juu viambishi –w-, -ik-, -i-, -an-, -eni-, vinaonesha kauli mbalimbali.

Katika isimu ya Kiswahili, pana kiambishi muhimu " h-" ambacho hutumiwa sana katika uwanja wa sarufi na katika mazungumzo ya kawaida. Uzito wa umuhimu wa kiambishi hiki, yaani ni muhali kukosekana kutumiwa kwenye mazungumzo yenye kuonesha hali ya ukanushi. Kiambishi " h-" hakina budi kiwemo, hasa katika baadhi ya nafsi zinapotumika. Hapa twafafanua kwa mifano ambayo yaweza kuthibitisha maelezo hayo.

Katika maandishi kwa mfano, kiambishi nafsi na kile kiambishi cha wakati si lazima kudondoshwa hata kama pana msururu wa viambishi vilivyofuatana ndani ya neno moja katika sentensi , Hebu tuchunguze sentensi zifuatazo:

i) Baba **a-na**-soma
ii) Baba **a-li**-kuwa **a-ki**-soma
iii) Baba **a-li**-kuwa **a-ki**-penda kusoma

Kupitia sentensi za hapo juu (i-iii) kiambishi **"a-"** katika kila sentensi ndicho kitendakazi chenye kuiwakilisha nafsi ya tatu umoja. Ilhali, kiambishi kilicho kati ya vistari viwili (-) katika sentensi zote hutenda kazi ya kuonesha matumizi ya wakati uliopo **"-na-"** na pia wakati uliopita **"-li-"** na wakati uliopita endelevu **"-ki "**

Tunachojifunza ni kwamba katika sentensi ya tatu (iiii), kiambishi cha nafsi na kiambishi cha wakati kwenye neno 'kusoma', vyote kwa pamoja vinafuatana. Bila shaka tukidondosha viambishi hivyo kwenye kitenzi cha mwisho, sentensi itakosa usanifu na usahihi wa kiumbo na hata kimaana. Lakini kinachozingatiwa hapa ni kuonesha tu kuwa viambishi vina uzito wake kwenye matumizi ya kiisimu.

Lakini kwa upande wa kiambishi " h-" hakina budi kitumike hasa katika matumizi ya kiisimu yenye kuonesha hali ya ukanushaji. Ndiyo maana kiambishi hichi husemwa kuwa ni kiambishi muhimu katika matumizi ya lugha ya Kiswahili wakati wa kusema au/na kuandika. Pasi na kutumika kiambishi " h-" dhana ya ukanushaji yaweza kukosekana katika nafsi zote za Kiswahili isipokuwa katika wa Nafsi ya Kwanza Umoja kama inavyodhihirishwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 3: Kiambishi **"h-"** katika hali ya Ukanushi

Hali Yakinishi	**Hali Kanushi**
Ninasoma	**Si**som**i**
Unasema	**H**usem**i**
Anasoma	**Ha**som**i**
Tunasoma	**Ha**tusom**i**
Wanasoma	**Ha**wasom**i**

Katika **Jedwali 3** hapo juu Kiambishi **"h-"** kinaonyesha hali ya ukanushi

Ispokuwa katika Nafsi ya Kwanza Umoja (**Si-**) katika wakati uliopo. Kutokana na uzito huo ndipo utafiti huu ulipoibuliwa ili kuchunguza matumizi ya kiambishi hicho katika miktadha tafauti. Wazo la mtafiti ni kuwa kiambishi hicho kinaweza kuwa na kazi zaidi ya hizo zilizioneshwa katika maandiko mbalimbali ya kiisimu. Ni muhimu pia kuzitafuta na kuzibainisha.

1.2 Suala la Utafiti

Katika kuitalii Sarufi ya Kiswahili inadhihirika kuwa yapo maneno ambayo huundwa kwa kuunganisha vipashio. Vipashio hivyo ndivyo wanaisimu wanavyoviita mara nyingi Mofimu. Makusudio ya kutaja mofimu hapa ni kwamba viambishi vya sarufi ya Kiswahili hukamilisha neno kiisimu. Yaani, kila kiambishi huwa kinasimamia dhana ya kisarufi. Mathalani, neno **'anasoma'** lina mofimu tatu kama ifuatayo:

a- nafsi
-na- wakati
-som- mzizi wa maana ya neno
-a kiambishi tamati

Halikadhalika, katika kutalii Vitenzi Halisi vya Kiswahili inadhihirika kuwa aghalabu ujenzi wa maneno yake hauna kiambishii mahsusi ambacho kinatambulisha hali ya uyakinishi. Mathalani, maneno kama vile '**a**naimba', '**tu**nacheza', '**m**nakula', '**u**nasema' na '**wa**nakimbia', yote kwa pamoja yameanzia na viambishi nafsi.

Yaani hupati kuona kuwa kabla ya kiambishi nafsi cha neno husika kuwa pana kiambishi kingine chenye kuelekeza hali ya uyakinishi. Lakini katika hali ya ukanushi maneno hayo huanza na kiambishi " h-" katika nafsi zote isipokuwa nafsi ya kwanza, umoja kama inavyoonekana hapa chini.

Jedwali 4: Nafasi ya kiambishi " h-" kama kikanushi kwenye neno

Hali Yakinishi	Hali Kanushi
Ninasoma	**S**isomi
Tunasoma	**H**atusomi
Unasoma	**H**usomi
Mnasoma	**H**amsomi
Anasoma	**H**asomi

Kwa mifano iliyomo katika **Jedwali la 4**

hapo juu ambayo inarejelea kwenye nafsi zote za Kiswahili, inadhihirika kwamba kiambishi " h-" ndicho kiambishi msingi kinachotumika katika ukanushi kwenye Kiswahili. Haidhuru nafsi ya kwanza (umoja) ukanushi wake uanze na /si-/, lakini mabadiliko hayo hayaghilibu sifa kuu ya kiambishi " h-" kuwa ni kiambishi cha ukanushi wa Kiswahili. Hali hiyo basi, ndiyo iliyokuwa asisi ya mada hii kutokana na umuhimu mkubwa wa kiambishi " h-" kuwa kama kiangamwa cha lugha hii katika ukanushi. Hivyo, mbali ya matumizi hayo ambayo hukitambulisha kiambishi " h-" kama kiambishi msingi cha ukanushi, utafiti huu ulichunguza pia matumizi mengine ya kiambishi" h-" yanayopatikana katika sarufi ya Kiswahili mathalani katika kioneshi, umbo kubalifu la neno na nafsi.

1.3 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya jumla ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza matumizi ya kiambishi "h-" katika sarufi ya Kiswahili. Pamoja na madhumuni hayo, utafiti ulikuwa na malengo mahsusi yafuatayo:

1.4 Madhumuni Mahsusi

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi yafuatayo:

i) Kubaini umbo la kiambishi " h-" kama mofimu katika maneno ya Kiswahili.
ii) Kubainisha nafasi inamotokea kiambishi " h-"katika maneno ya Kiswahili.
iii) Kubainisha uamilifu (utumikaji) wa kiambishi " h-" katika lugha ya Kiswahili.

1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti umefanyika kwa kutumia maswali yafuatayo:

i) Je, kiambishi" h-" kina maumbo yapi kama mofimu katika maneno ya Kiswahili?
ii) Je, kiambishi " h-" hutokea katika nafasi zipi katika maneno ya Kiswahili?
iii) Je, kiambishi " h-" kina uamilifu (utumikaji) upi katika lugha ya Kiswahili?

1.6 Mawanda ya Utafiti

Sarufi ya Kiswahili ina viambishi kadhaa ambavyo hutokea mwanzoni na baada ya mzizi wa neno. Vipashio hivyo shurti vibebe maana ya kisarufi.

Katika aina za maneno ya Kiswahili mengi yana viambishi. Kwa mfano, majina ya vitu, hasa majina yaliyo yaliyomo katika hali ya umoja na wing,vivumishi au/na viwakilishi, vielezi pamoja na vitenzi. Viambishi hivi huoneshwa kwa msingi wa Ngeli za majina kama hivi inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo,

Jedwali 5 Viambishi katika aina za maneno .

Aina ya neno	**Mfano (kabla ya mabadiliko)**	**Mfano (baada ya mabadiliko)**	**Kiambishi Ngeli au** upatanishi
Nomino	Mtu	Watu	M- / WA-
Kivumishi	Kizuri	Vizuri	KI-VI
Kiwakilishi	Huyu	Hawa	YU/A-WA
Kielezi	Hapa Hapo Humo	Hapa Hapo Humo	Mahali
	Hiki Hicho Kile	Hiki Hicho Kile	Masafa/umbali

Zifuatazo ni sababu chache ambazo zinajibu swali muhimu la kwa nini kilitafitiwa kiambishi hiki tu " h-" na wala siyo kiambishi kingine. Kwanza, kiambishi " h-" hubeba wajibu mkubwa wa kubadilisha hali ya ukanushi. Ilhali hatupati ubadilishaji kama huo kwenye hali ya uyakinishi. Kutokana na uzito huo tunadhani kuwa kiambishi hicho kina nguvu za kisarufi ishindayo viambishi vingi katika sarufi ya Kiswahili.

Pili, kiambishi " h-" aghalabu hukaa mwanzoni mwa neno. Jambo hili nalo limekuwa sababu ya kutaka kujua kwa nini iwe hivyo. Ndiyo sababu utafiti huu ulichunguza kwa kina juu ya nafasi ya kiambishi hiki katika neno.

Pamoja na sababu hizo, utafiti umefanyika zaidi katika mazingira ya lugha ya Kiswahili. Kiambishi " h-" huweza kutokea katika maneno ya lugha ya Kiswahili kuonesha dhana zisizofanana kwa mfano viambishi Ngeli, vioneshi mahali, masafa n.k.

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti wa kiambishi " h-" una muhimu kufanyika kwa kuwa tulitaka kutambuwa matumizi kadha wa kadha ya kiambishi hicho kwenye Sarufi ya Kiswahili. Iliaminika kwamba licha ya uamilifu (utumikaji) wake wa ukanushi, kiambishi hicho kinayo matumizi mengine. Hivyo, kufanyika kwa utafiti huu kumetuwezesha kuyatambua matumizi hayo mengineyo ili hatimaye iwe ni mchango mpya katika ongezeko la matumizi ya kiambishi hicho. Pamoja na umuhimu huo utafiti huu pia umesaidia katika mambo yafuatayo:

Kwanza, ni kwa wahadhiri na wanafunzi wa vyuo vikuu, unawasaidia katika kupata utambuzi wa matumizi kadhaa wa kadha ya kiambishi " h-" Utambuzi wa matumizi mengineyo ya kiambishi hicho utaleta faida kwa wataalamu wa sarufi ya lugha ya Kiswahili, kuwasaidia katika uundaji wa maneno mapya.

Pili, utafiti huu umeweza kugundua mabadiliko kadhaa ya lughawiya (isimu); hasa mabadiliko yahusuyo viambishi na uambishaji. Mfano mmojawapo wa mabadiliko hayo ni pale umbo h- linapobadilika kuwa umbo **Si**- wakati nafsi ya kwanza (umoja) inapofanyiwa uambishaji kutoka hali Yakinishi kwenda hali Kanushi. Katika kusoma kazi za awali, yamegundulika makosa ya tafiti kadhaa zilizotangulia ambazo zilihitimishwa kwa kutotilia uzito wa kiambishi "h-" katika matumizi sahihi mengi ya Kiswahili.

Tatu, utafiti huu ni muhimu kwa kuwa utakuwepo katika maktaba za kitaaluma kama marejeleo na msingi wa kufanyia utafiti zaidi . Tutambue kuwa kumbukumbu nyingi za sarufi zinazidi kupungua kwa sababu watafiti wengi wanaelekea kushawishika kufanya utafiti kwa mada za fasihi kuliko zile za sarufi.

1.8 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika kuchunguza lughawiaya (isimu) ya sarufi ya Kiswahili Sanifu na umechunguza matumizi ya kiambishi " h-". Lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi. Utafiti huu umehusu lugha ya Kiswahili Sanifu zaidi.

SURA YA PILI

USOMAJI WA MAANDISHI TANGULIZI

2.0 Utangulizi

1. Sura hii inawasilisha Usomaji makini uliofanywa kuhusu mada ya viambishi, hasa kiambishi ‘h-‘. Kazi hizo siyo tu zilikuwa dira ya maeneo kadhaa kwa utafiti huu, bali pia , zilibainisha pengo ambalo lipo katika matumizi ya kiambishi" h-" kwa mujibu wa sarufi ya Kiswahili Sanifu.

2.1 Nadharia ya viambishi kwa jumla

Mdee (1996) anakifafanua kiambishi kwa kusema kuwa ni mofimu inayowekwa kwenye mzizi wa neno au/na kukamilisha muundo wa neno. Mdee (mtajwa) ana wazo kuwa uambishaji unaweza kutokea kabla au baada ya mzizi wa neno. Wazo hilo kwa maoni ya mtafiti lina mashaka fulani. Kwa sababu taaluma ya sarufi ya Kiswahili mara nyingine huweka bayana kwamba zile mofimu zinazokuja baada ya mzizi wa neno huitwa mofimu za mnyambuliko. Mambo mawili hayo; uambishaji na mnyambuliko, kila moja lina dhima mahsusi. Kwa mfano, Mdee (mtajwa) anaitaja aina ya kwanza iitwayo ‘viambishi viambatanishi ambavyo ama huambatanishwa kwenye mzizi wa neno ama kwenye viambishi vingine vya neno. Hata hivyo, Mdee anasema kuwa uambishaji huo unapotokea, huwa haubadilishi kategoria ya neno wala haupotezi maana ya neno hilo. Ichunguze mifano ifuatayo.

i) Mtoto [wa]toto,
ii) Kisu [vi]su
iii) Embe [θ]embe

Katika mifano hiyo tunadhihirikiwa na mambo mawili. Mosi, kutobadilika kwa maana ingawa pana uambishaji uliotendeka. Pili, maneno yaliyoambishwa yameendelea kubaki kwenye aina ileile ya kundi Ngeli. Mabadiliko pekee yanayoonekana kwamba kila nomino imetoka hali ya Umoja na kuwa hali ya Wingi. Mnasaba huo basi umetufanya tuone kuwa dhima mojawapo ya uambishaji ni kuibadilisha nomino kutoka katika umoja kwa wingi. Halikadhalika, tunaweza kusema kwamba uambishaji pia una dhima ya kuonesha mofimu za uoneshi na katika kuunda neno kama itkavyodhirika katika sura zijazo za andiko hili. Na hivyo, mwanasarufi hubaini kuwa baadhi ya nomino huwa na umbo tegemezi kama ilivyojitokeza kwenye mfano wa (i) na (ii) hapo juu. Vilevile kwa mifano hiyo, mwanasarufi huona bayana mwachano wa viambishi ambatishi na mzizi vilivyoambatana nao. Ilhali katika mfano wa (iii), hapana uwazi unaojitokeza wa kiambishi ambatanishi. Hata hivyo, inajulikana tu kuwa kipo kiambishi katika sura ya ufiche (θ)

Aina ya pili ni ‘viambishi nyambuaji.’ Hivi hutenda kazi ya kujenga au kuunda maneno mapya. Mdee (1996) anasema kuwa viambishi hivyo huambatanishwa kwenye mzizi wa neno na kujenga neno jipya lenye maana tofauti na leksimu sahili. Katika aina hiyo amesema kuwa aghalabu husababisha kategoria ya neno kubadilika. Mifano ifuatayo inaonesha unyambulishi unavyobadili katagorea za maneno

i) Cheza - kitenzi mchezo, mchezaji, mchezeshaji (nomino)
ii) Lima – kitenzi kilimo, ukulima, mkulima (nomino)

Mifano hiyo inaonesha mambo mawili: Mosi, mabadiliko ya kitenzi kuwa nomino baada ya unyambulishaji kufanyika. Lakini pili, nomino zilizopatikana hazijikiti katika ngeli moja tu. Zinajikita katika ngeli kadhaa kma mehezo (ma-/mi-) mchezaji (m-/wa-) kilima (ki-/vi-) ukilima (u-/u-) mkulima. Hivyo, hapa, tunajifunza kwamba unyambulishaji wa vitenzi ni njia mojawapo inayounda maneno mapya ambayo mara nyingi huingia kwenye Ngeli tofauti. Nayo

majina yenyewe yanaweza kuwa na sifa ya utendaji kama lilivyo neno 'mchezaji'. Lakini pia yanaweza kuwa ni katika sifa ya utendeshaji kama lilivyo neno 'mchezeshaji'. Hata hivyo, mabadiliko yanayoonekana hapo juu yamepata usaidizi wa mchakato wa uambishaji ambao, kwa tabia yake. hufanyika kabla ya mzizi. Kwa sababu maneno yote yaliyopo hayaonekani kupata mabadiliko kule mwishoni pekee (baada ya mzizi). Bali yamechanganya. Kwa mfano:

cheza+ mcheza+mchezaji+wachezeshaji

lima-kilimo-mkulima, ukulima, ulimaji

Katika kuendeleza uchambuzi wa viambishi, Mdee (mtajwa) amebainisha pia kama inavyodaiwa na baadhi ya wataalamu wa sarufi. kuwa Kiswahili hakina kiambishi kati. Hapa anakusudia kufanya ukosoaji wa mgawanyo wa aina tatu za viambishi (awali, kati na tamati) kama baadhi ya kazi za sarufi zilivyobainisha. Wazo la Mdee (mtajwa) ni kwamba viambishi kati ni vile tu ambavyo vitatokea **ndani ya mzizi** wa neno na ambavyo huweza kubadilika pale neno linapobadilika kutoka hali ya umoja na wingi kama vile ilivyo kwenye lugha ya Kiingereza "man – men".

Mdee anatoa mifano mingine ambayo ndani yake kimo kiambishi " h-". Mifano hiyo inapatikana kwenye vile anavyoviita 'vivumishi na viwakilishi vioneshi. Mifano aliyoiweka ni kama vile ***h****iki,* ***h****icho,* ***h****uyu,* ***h****uyo,* ***h****apo,* ***h****apa,* *hao,* ***h****ii,* ***h****izi,* ***h****awa,* ***h****umo,* ***h****ili* na ***h****ilo*.

Vilevile Mdee (mtajwa) ameonesha matumizi ya kiambishi " h-" anapofafanua alama za njeo (wakati) katika kitenzi. Inawekwa mifano kwenye Jedwali lifuatalo ili ionekane namna kiambishi hicho kinavyotumika kwenye vitenzi kikiwa na dhima maalumu.

2. **Jedwali 6:** Matumizi ya Kiambishi " h-" katika nafsi katika nyakati tofauti

Wakati uliopo		
Nafsi	Yakinishi	Kanushi
I – Umoja	Ninaimba	Si-imbi
III – Umoja	Anakimbia	Ha-kimbii
II – Wewe	Unasoma	Hu-somi
III – Wingi	Wanasimama	Ha-wasimami
Wakati uliopita		
II – Umoja	Ulisoma	Hu-kusoma
III – Umoja	Alikimbia	Ha-kukimbia
III – Wingi	Walilima	Ha-wakulima
I – Wingi	Tulilima	Ha-tukulima
Wakati Ujao		
II – Umoja	Utasoma	Hu-tasoma
III – Umoja	Atakimbia	Ha-takimbia
I – Umoja	Nitaimba	Si-taimba
III – Wingi	Watasimama	Ha-watasimama

Kihampa, (2003), amefanana na Mdee (1996) katika utumiaji wa kiambishi " h-" wakati wakibainisha mgawanyo wa aina za maneno. Wamekitumia kiambishi hicho pale walipotoa mifano ya vivumishi vioneshi pamoja na mifano ya viwakilishi vioneshi. Wataalamu hawa wameeleza kuwa kiambishi hiki hutumika katika ubainishaji wa 'hali isiyodhihirika' ambayo hupatikana katika wakati uliopo. Katika mifano ya ufafanuzi wao wamesema kuwa hali hiyo desturi yake ni kuanza kwa kiambishi [hu] katika maneno yake. Kwa mfano,

i. Shaaban **hu**cheza mpira

ii. Maryam **hu**watembelea wazazi wake kila mwaka.

Kwa mifano hiyo, inaonekana bayana kuwa kiambishi " h-" kinatenda kazi ya kuonesha hali ya mazowea ambayo akina Kihampa (mtajwa), wao wameiita 'hali isiyodhihirika'. Mifano hiyo bila shaka imemsaidia mtafiti katika utambuzi mmojawapo wa matumizi ya kiambishi " h-".

Rubanza (2003), katika kuzungumzia viwakilishi vioneshi amepiga hatua zaidi kwa kuweka tafauti ya maneno yatumikayo katika kuonesha masafa baina ya mzungumzaji na msikiaji. Amesema kuwa iwapo mtajwa yuko karibu na mzungumzaji basi vioneshi 'huyu' na 'hawa' hutumika. Lakini iwapo mtajwa yu karibu na msikilizaji basi vioneshi 'huyo' na 'hao' hutumika.

Jedwali 7: Viwakilishi Vioneshi vya masafa

MASAFA	UMOJA	WINGI
Karibu na msemaji	Huyu	Hawa
Karibu na msikiaji	Huyo	Hao
Mbali na msemaji na msikiaji	Yule	Wale

Katika kazi hii tunajifunza kwamba hivyo vionyeshi ingawa vyote hutenda kazi ya ukaribu, lakini hutafautiana kimatumizi. yaani, kila kionyeshi hufungamana na muktadha maalumu wa utumizi wake kulingana na masafa kati ya mzungumzaji na msikilizaji. Ufafanuzi huu wa Rubanza (mtajwa) ulichukuliwa kama njia mojawapo katika kutafautisha matumizi ya kiambishi " h-" ilhali matumizi hayo asili yake ni kutokana na hali ya ukaribu.

Khamis (2011) katika kuizungumzia dhana ya viambishi amesema kuwa 'Kiambishi ni kipande cha neno kilichoambatanishwa kwenye mzizi au kiini cha neno na chenye kuainisha kazi mahsusi ya kisarufi. Maandishi hayo yamekuwa dira iliyoongoza kufahamu kwamba kiambishi katika neno huwa na dhima maalumu. Hivyo basi, ikitokea kipande fulani cha neno hakitoi maana ya lughawiya (isimu), hicho hakiwezi kupewa hadhi ya kiambishi. Katika utafiti huu pale " h-" ilipotumika kama kiambishi, imeleta maana mahsusi. Na pale ambapo haikuleta maana maalumu, basi, ilichukuliwa kama umbo maalumu la kiambishi linalobeba dhima maalumu isiyokuwa ile ya kiambishi kwenye neno hilo. Maneno ya Khamis (mtajwa) yanaonesha kuwa kiambishi cha ukanushi aghalabu hujitokeza kwenye ukanusho wa nafsi.

Uchunguzi zaidi umeonesha kuwa Khamis (mtajwa) anatafautiana na baadhi ya wataalamu wenzake katika dhana ya vioneshi. Anadai kuwa hakuna Vivumishi vionyeshi na badala yake kuna vibainishi vioneshi. Hata hivyo, viambishi vitumikavyo kwenye vibainishi vioneshi ndivyo vilevile ambavyo pia huitwa 'Vivumishi vioneshi. Katika hali yoyote iwayo, kwenye utafiti huu tafauti hizo hazikuwa na umuhimu wa pekee. Kihore na wenzake (2012) wamesema kuwa 'viambishi ni mofimu zinazoambatanishwa kwenye mzizi wa neno ili kuwakilisha hali au dhana mbalimbali zinazofungamana na neno.' Pamoja na mofimu hizo wameendelea kusema kuwa katika lugha ya Kiswahili viambishi huweza kujitokeza tu mwanzoni au mwishoni mwa mzizi. Wakati huohuo katika kuzungumzia viambishi vya njeo (wakati) katika hali ya ukanushi,wameonesha kuwa kiambishi "h-"hutumiwa katika wakati uliopita kama vile [ha-kulia], wakati uliopita hali timilifu kama vile, [ha-tujala] na wakati uliopo kama vile [ha-tuli]. Katika wakati ujao kiambishi hicho pia hujitokeza. k.m. hatutasoma Vilevile, wameonesha kuwa kiambishi [ha-] kinatumiwa pia katika kukanushia kitu. Kwa mfano, [ha-kijaiva]. Papo hapo wameeleza kuwa kiambishi "h-" hutumiwa katika kuonesha hali ya mazowea. Kwa mfano:

Yeye <u>hu</u>-tembelea.

Mambo <u>hu</u>tokea

Sisi <u>hu</u>furahi n.k

Kupitia mchango huo tumepata kuona namna kiambishi " h-" kinavyotumika kama kikanushi katika njeo (wakati) mbalimbali. Zaidi ya hivyo tumeona kwamba kiambishi hiki kwa tabia yake hufungamana pamoja na kiambishi cha nafsi ili mkanushaji au mkanushwaji awe bayana. Hivyo basi kazi ya akina Kihore (mtajwa) nayo imeendeleza kutufunza kwamba kiambishi " h-" ni kiambishi muhimu kwa dhana ya ukanushi.

3. Kindly (1986) kwa upande wake amesema kuwa kiambishi ni silabi ipachikwayo kwenye mzizi au kiini cha neno. Nacho kina uwezo wa kubadili maana ya neno'. Kindly anaamini kuwa viambishi ni vya aina tatu; yaani, Viambishi Awali, Viambishi Kati na Viambishi Tamati. Kwa ufafanuzi huo, ni dhahiri kwamba kiambishi siyo silabi yoyote tu ipatikanayo katika neno, ni sharti silabi hiyo iwe na matumizi maalumu. Ndiyo maana Kindly (mtajwa) amesisitiza kuwa silabi hiyo maalumu inayo tabia ya kubadili maana ya neno. Inatupasa tuwe waangalifu na jinsi Kindly (mtajwa) anavyoielewa 'silabi' – si katika masuala ya utamkaji bali katika kazi yake ya kisarufi.

Maelezo ya Kindly (mtajwa) yanasaidia katika mambo mawili makuu. Mosi, wataalamu wa sarufi wanayo mitazamo tofauti katika uainishaji wa aina za viambishi. Yaani, baadhi yao huchukua kigezo cha mzizi kuwa ni kama 'mpaka' wenye kubainisha aina zenyewe. Katika mtazamo huo, vile viambishi vyote ambavyo hutokea kabla ya mzizi wanavifasiri kuwa ndivyo Viambishi Awali. Ilhali vile viambishi ambavyo hutokea baada ya mzizi, vyote kwa pamoja huwa ni Viambishi Tamati. Hata hivyo, wapo baadhi yao wanaoamini kuwa Kiambishi Awali ni kile tu kinachojitokeza mwanzoni mwa neno sawa

na kiambishi tamati/mwisho ambacho nacho ni kile chenye kujitokeza mwishoni mwa neno. Na vile vyote ambavyo vipo baina ya Kiambishi Awali na Kiambishi Tamati, hivyo huitwa Viambishi Kati.

Masebo na Nyangwine (2002), wamekizungumzia kiambishi " h-" kama kioneshi na kama kikanushi. Hizo ni miongoni mwa dhima muhimu ambazo kiambishi hicho huzitenda kwenye maneno au/na sentensi za Kiswahili. Kusema kweli kazi yao hiyo imekuwa ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu nayo imeendeleza utambulishaji wa dhima za kiambishi " h-" ambazo baadhi ya kazi tangulizi zimeshaweka wazi kama ilivyodhirishwa na Mdee (mtajwa). Hapa ni vyema kubainisha kwamba huo msisitizo wa wataalamu kadhaa (Mdee, Rubanza, Kihore na wenzake) kuzirudiarudia dhima hizohizo kwenye kazi tangulizi zao ndilo jambo ambalo limemjaza hamasa mtafiti huyu katika kufanya utafiti huu ili kuchunguza iwapo yapo matumizi mengine ya kiambishi " h-" katika lugha ya Kiswahili.

Batibo (2010), amevigusia viambishi (japo kwa kifupi) wakati alipowasilisha mada ya 'Uchunguzi Katika Sarufi ya Kiswahili na Lugha Zinazohusiana'. Kwa uwasilishaji huo amezungumzia namna mpangilio wa viambishi ulivyo kwenye lugha za Kibantu na kwamba huwa ni wa aina ama ya muundo wa KI- au IKI-. Muundo wa KI- hapo ni ule muundo unaotambulikana kama muundo wa 'Konsonanti-Irabu'. Yaani, ujenzi wa neno la lugha ya Kibantu yoyote huanza kwa konsonanti na kufuatiwa na irabu kama ilivyo kwenye neno ***pipa,kaka, dada….n.k*** . Kumbe kwa miundo hiyo, na kwa vile Kiswahili (hadi sasa) kinakubalika kuwa ni miongoni mwa lugha za kundi la Kibantu, basi ni dhahiri kuwa kiambishi "h-" ni miongoni mwa mihimili mikuu ya maneno ya Kiswahili kama kinavyobainikakimebainika kuwa katika miundo iliyotajwa. Yaani, mara nyingi hupatikana kwa kuunganisha konsonanti na irabu, (kwa mfano: ba+ba = baba, da+ka = dada) ilhali mara nyingine hujitokeza kama irabu inayojitosheleza (kwa mfano: u+a = ua, o+a = oa). Msingi huo wa miundo hiyo ndiyo uliotuelekeza katika kuyafahamu matumizi kadhaa ya kiambishi " h-" yanayojitokeza kwenye miktadha tofauti. Aidha, Batibo (mtajwa 2010) amezidi kusema kwamba viambishi awali vya Ngeli hutumika pia katika kuleta mnyambuliko wa kimsamiati. Pamoja na ufafanuzi huo nikiri kuwa kazi ya Batibo (mtajwa) msaada mkubwa kwenye utafiti huu. Kwa sababu imeweza kuleta usaidizi katika kumuongoza mtafiti namna ya kuchambua kazi za viambishi vya lugha ya Kiswahili.

Kazi nyingine iliyodurusiwa katika utafiti huu ni ile ya Mkude (2010). Kupitia kazi hiyo kumezungumziwa kiambishi " h-" kama mofimu inayotenda kazi ya kuonesha hali ya mazowea. Yaani, kiambishi hicho kinapotumika mwanzoni mwa vitenzi, baadhi ya wakati huwa kina kazi ya kuonesha hali ya mazowea. Hali hii ya mazowea mara nyingi hutumia nafsi bila kuitaja bayana. Mfano ni kama kusema:

(wao) *h*uimba,

(sisi) *h*ucheza

(yeye) *h*ulia , n.k.

Ifahamike kuwa neno 'mazowea' hapa linakusudiwa kuonesha desturi ya mtu, jambo linavyofanyika mara kwa mara kwa mfano kila siku, au kila juma, au kila mwezi au kila mwaka, na kadhalika. Bila shaka kazi hii ya Mkude mtajwa ilikuwa mchango mkubwa katika utafiti huu.

Msanjila (1985) amekizungumzia kiambishi" h-" na kukipatia kazi mbili. Kazi ya ukanushi na nyingine ni kazi ya kubainisha upatanishi wa maneno kwenye sentensi. Hii imedhihirishwa katika mifano ifuatayo:

Kutokana na kazi hii mtafiti kwa mara nyingine ameweza kunufaika kwa kupata matumizi mapya ya kiambishi kilichotafitiwa; matumizi ya upatanishi wa maneno. Kusema kweli kabla ya kufanyika utafiti huu mtafiti hakuwahi kudhani kuwa kiambishi " h-" kinayo matumizi ya namna hiyo. Dhima ya upatanishi wa kisarufi ni dhima muhimu sana kwenye lugha. Ifahamike kuwa ushindikanaji wa matumizi ya upatanishi wa kisarufi kwenye sentensi au tungo yoyote iwayo, huleta utata wa kimaana. Hivyo pale kiambishi" h-" kikosekanapo kutumika mahala hapo kitaleta dosari ya sentensi au tungo kutofahamika vyema Kwa minajili hiyo ndipo makala ya Msanjila (mtajwa) ilipoleta tija kwa utafiti huu kwa sababu mtafiti aliweza kupiga hatua mbele katika utambuzi wa matumizi ya kiambishi"h-" alichokitafiti.

Alzarouk (2010) amevitaja viambishi njeo (wakati) vya sarufi ya Kiswahili kuwa vipo katika namna mbili; yaani, yakinishi na kanushi. Viambishi yakinishi ni vile tu ambavyo vinabainisha hali ya kukubalika jambo. Wakati viambishi vya ukanushi hutumika katika kubainisha hali ya kukataa jambo au kitu.

Mohamed (2013) anakisawiri kiambishi " h-" kama msingi wa ukanushaji katika Kiswahili. Kiambishi hiki ni cha msingi kwa sababu ndicho kiambishi pekee chenye nafasi kubwa kwenye ukanushaji unaojitokeza katika sarufi ya Kiswahili. Jambo moja lililo zito ambalo Mohamed (mtajwa) amelizungumzia ni mabadiliko ya umbo la neno yanayotokea pale kiambishi " h-" kinapofungamana na kitenzi. Yaani, mwishoni mwa kitenzi hicho mara nyingi ile irabu inayomalizia huwa katika umbo la –i- au –a- tu na hivyo kuifanya asili ya umbo kupokea mabadiliko mwanzoni na mwishoni. Mabadiliko haya ambayo yamezungumziwa na mtafiti huyo yameleta msaada mkubwa kwa utafiti huu katika kupiga hatua ya upatikanaji wa matumizi ya kiambishi " h-" kwenye sarufi ya Kiswahili kama ilivyoelezewa kwenye Uwasilishaji wa data wa utafiti huu. Ifahamike tu kuwa ubadilikaji wa umbo la neno linalohusika, kila ulipotokea ulitokana na njeo (wakati) iliyotumika kwenye kitenzi chenyewei la hapa chini limenukuliwa kwenye kazi ya Mohamed (mtajwa) ili litubainishie namna kiambishi cha ukanushaji " h-" kinavyobadili umbo la neno mwishoni mwa vitenzi kulingana na njeo (wakati) iliyomo.

Jedwali 8: Vikanushi katika Njeo (wakati)

	Kitenzi	Hali ya ukanushi			
		Wakati uliopo	Wakati uliopita	Wakati ujao	Wakati/hali timilifu
Nafsi ya Kwanza (umoja)	-pika	Sipik*i*	Sikupika	Sitapika	Sijapika
Nafsi ya Kwanza (wingi)	-pika	*Ha*tupik*i*	Hatukupika	Hatutapika	Hatujapika
Nafsi ya Pili (umoja)	-pika	*Hu*pik*i*	Hukupika	Hutapika	Hujapika
Nafsi ya Pili (wingi)	-pika	*Ha*mpik*i*	Hamkupika	Hamtapika	Hamjapika
Nafsi ya Tatu (umoja)	-pika	*Ha*pik*i*	Hajapika	Hatapika	Hajapika
Nafsi ya Tatu (wingi)	-pika	*Ha*wapik*i*	Hawajapika	Hawatapika	Hawajapika

Mifano ya hapo juu yabainisha kuwa ukanushi katika vitenzi vya Kiswahili aghalabu utumikapo na wakati au halikiambishi " h-" hutangulizwa kwenye mzizi wa kitenzi husika.. katika wakati uliopo huishia na irabu –i.Lakini katika nyakati zilizobakia, irabu –a haibadiliki. Hata hivyo, Jedwali hilo, linaonesha kuwa itumikapo katika Nafsi ya Kwanza (umoja), kiambishi " h-" hubadilika na kuchukua umbo la /si-/

Utafiti wa Mohammed (mtajwa) umeonesha upatikanaji wa matumizi ya kiambishi "h-" hasa pale kinapofungamana na kitenzi. Kazi hiyo ya Mohamed imetubainishia namna kiambishi hicho kinavyoweza kulibadili umbo la kitenzi kulingana na matumizi ya njeo (wakati) inayotumika.

Habwe na Karanja (2004) wamefafanua matumizi ya kiambishi " h-" kuwa ni kiambishi cha ukanushi na kinapoingia kwenye sentensi huwa kinasababisha utata mifano . Wataalamu hao si kwamba wanabainisha matumizi ya kiambishi hicho tu,, bali pia wanadhihirisha athari ya kimaana pale inapotokea kiambishi hicho kuingia kwenye kitenzi cha sentensi. Wataalamu hao kwa kutumia kazi hiyo wanadai kuwa sarufi ya Kiswahili inayo viambishi viwili tu vya ukanushaji- /si-/ na " h-". Madai yao yanazingatiwa katika utafiti huu na kwamba imebainika kuwa viambishi hivyo vinayo nafasi kubwa katika ukanushaji kwenye sarufi ya Kiswahili. Ifahamike kuwa kazi ya wataalamu hao imesaidia katika kuzidi kudhihirisha utafiti huu kuwa kiambishi" h-" matumizi yake makuu ni ukanushaji. Ifahamike kuwa lugha ni pande mbili zenye kutegemeana. Hali yakinishi na hali kanushi. Hivyo ni dhahiri kabisa kwamba endapo hali kanushi ikikosekana, kiwakilishi cha ukanushaji, usahihi katika lugha hiyo itayumba.

Mgullu (2010) katika kuizungumzia dhana ya viambishi amesema kuwa viambishi huonesha sehemu za maneno ambazo huambishwa-katika mizizi ya maneno. Mgullu (mtajwa) amevigawa viambishi katika aina tatu kuu. Yaani, viambishi awali, viambishi ndani na

viambishi tamati. Mgullu amekitumia kiambishi "h" kama mofimo oneshi katika aina za vivumishi na viwakilishi.

Ali (2015) katika utafiti alioufanya kuhusu lahaja mbili za Kisiwa cha Pemba yaani Kiswahili cha Chakechake na Kiswahili cha Micheweni.amebaini kuwa pale ukanushaji unapofanyika, umbo /si-/ ambalo hutumika kwenye Kiswahili Sanifu hubadilika na kuwa umbo /se-/. Ifahamike kuwa umbo /si-/ ni aina ya umbo la kiambishi " h-" ambalo mara nyingi hutumika pale inapotumika nafsi ya kwanza, umoja tu.

Jedwali 9 Ukanushaji Katika Ki-Micheweni, Ki-Chake Chake na Kiswahili Sanifu

Kimicheweni	Kichakechake	Kiswahili Sanifu
Semuona	Sikumuona	Sikumuona
Haji	Hatokuja	Hatakuja
Hebu	Hataki	Hataki
Usende	Usiende	Usiende
Seepo	Sikuwepo	Sikuwepo

Katika Jedwali hilo mtafiti ameona ya kwamba hakuna tofauti ya kiambishi kanushi cha Kichakechake na Kimiicheweni kiumbo, isipokuwa tofauti iliyopo ni kwenye matamshi tu. Pili, kikanushi chake Kichakechake ndicho kilekile cha Kiswahili Sanifu. Hivyo, hapa utafiti umebaini kuwapo kwa athari kubwa ya matumizi ya Kiswahili sanifu katika baadhi ya miji mikubwa ya Pembai ukiwemo mji wa Chake Chake. Athari ya namna hiyo huenda ikiwa haikuzingatiwa vile ifaavyo na ipasavyo.

2. 3 Mikabala ya nadharia ya viambishi

Utafiti huu umetumia nadharia moja; yaani, Nadharia ya Uamilifu (utumikaji) pamoja na mkabala mmoja; yaani Mkabala wa Uchunguzi Tofautishi. Tunatoa ufafanuzi mfupi kuhusu kila kimoja cha vipengele hivi kama ifuatavyo:

2.2.1 Nadharia ya Uamilifu (Utumikaji)

4. Nadharia hiyo ni mwendelezo wa nadharia iliyoasisiwa na Charles Darwin itambulikanayo kwa jina la 'Evolution Theory' (Nadharia ya Mageuko) Nadharia iliyo bega kwa bega na nadharia hiyo ni ile ya Uamilifu iliyoanzishwa na Talcot Parsons (1902 – 1979). Kimsingi, nadharia hiyo inabainisha umuhimu katika utenda kazi wa kila kijenzi cha kiumbe. Kwa kifupi, nadharia hiyo inaelekeza kuwa katika kiumbe chochote kiwacho, kila kiungo chake lazima kina kazi maalumu. kinayoitenda. Tuchukue mfano wa mkono wa mwanadamu. Unaweza kusema mkono kama kiungo kina viungo vingine vidogovidogo ambavyo hutenda kazi pasipo kuingiliana ingawaje hushikamana katika utendaji huo ili kuhakikisha kuwa dhima nzima ya mkono linatekelezwa na kutimizwa. Mathalan, katika mkono kuna vidole, zipo kucha, kuna kiganja, kuna ngozi, na viungo vinginevyo. Katika viungo hivyo, kidole kinaweza kuwa na kazi ya kuonesha kitu mahali kilipo, kubainisha ishara fulani kama vile ishara ya wito au/na kushika na kukamatia kitu. Papo hapo kucha licha ya kushikana na kidole, hutenda kazi ya kupara au kukuna, yaweza kutumika kama silaha na kishikizo cha mapambo kama vile hina na rangi kadhaa. Kiganja kinayo kazi ya kupapasa, kuandaa kuashiria hisia au kushika kitu. Ngozi nayo hutumika kama kilinzi cha mishipa na nyama za ndani, kutolea hisia pamoja na kubainisha kabila/rangi ya mtu.

5. Bila shaka, lugha kama mfumo wenye mshabaha na kiumbe, unayo viungo/vijenzi viujengayo. Kwa mujibu wa Mgullu (2010) Katika mkabala wa lughawiya (isimu) pana matawi kama vile isimu historia, isimu fafanuzi, isimu linganishi, isimu jamii, isimu tumizi, isimu falsafa, isimu tiba na isimu nafsia. Katika upande mwingine, Mgullu (mtajwa) anaviorodhesha viwango vinne vikuu vya lugha: Fonolojia, Mofolojia, Sintaksia na Semantiki. Katika taaluma ya Mofolojia Kihore na wenzake (2012) wanakubaliana kuwa maneno ya Kiswahili yana vigawanyo vyake ambavyo ndivyo wanavyoviita 'aina/kategoria za maneno'. Miongoni mwa aina hizi za maneno zipo ambazo ndani yake hupatikana viambishi. Kwa sababu lugha ina mfungamano wa vijenzi vingi na kila kijenzi kina kazi zake. Utafiti huu umefanyika ili kuyachunguza matumizi ya kiambishi " h-" kwenye sarufi ya Kiswahili.

6. Pamoja na nadharia hiyo, utafiti huu ulitumia pia nadharia iitwayo Nadharia ya Mkabala wa Uchunguzi Tofautishi. Nadharia hii inadai kwamba kila kipengele kina nafasi yake mahususi katika neno na kutokana na vipengele hivyo kuunganika viwango vikubwa zaidi vya lugha kama vile sentensi hupatikana. Sababu za kuitumia nadharia hii ni kwamba hubainisha na kutofautisha kimaumbo na kikazi kiambishi " h-" na viambishi vinavyoshikana nacho ili kupata umbo la neno linalokubalika la Kiswahili.

7. 2.2.2 Mkabala wa Uchunguzi Tofautishi

Huu ni mkabala ambao wanalughawiati (wanaisimu) miongoni mwao Habwe na Karanja (2004) huurejelea wakati wanapofanya uchunguzi wenye kutafautisha masuala ya kisarufi. Kusema kweli mkabala huu unazo athari nyingi za nadharia kubwa zaidi ya 'Umuundo' iliyoasisiswa na Ferdinand de Saussure. Mikabala hii miwili ilitumika sana kwenye miaka ya 1940 hadi 1950. Pale wanafunzi walipojifunza lugha ya pili aghalabu walifunzwa kwa miongozo na misingi ya mikabala hiyo.

Tunafahamu kuwa mikabala hiyo ilitumika katika kutofautisha na kulinganisha lugha mbili zilizo tofauti. Kimsingi, msisitizo ulikuwa katika kuzitofautisha lugha au kuzigawa katika aina za kimuundo kwa kuihusisha sarufi yake – yaani Mofolojia, Fonolojia, Sintaksia na msamiati kwa pamoja kwa kuwa vyote kwa pamoja hutegemeana na kukamilishana kama vipengele vya lugha moja husika. Wala hauzingatii kabisa suala la historia tu ya lugha husika (Crystal, 2003). Kwa mnasaba huo, mkabala huu umesaidia katika kumuongoza mtafiti kuweza kutafautisha au/na kulinganisha kiambishi " h-" na viambishi vyengine.

2.3. Muhtasari

8. Katika udurusu huo wa kazi tangulizi tumeangazia mambo muhimu yanayostahili kutiliwa

maanani. Mosi, katika ukusanyaji data tafauti za maumbo na hata uamilifu wa kipashio umebainika. Pili, mtazamo huu umezingatia kwa usahihi na kwa uhakika zaidi madhumuni yaliyokusudiwa. Tatu, usomaji wa kazi tangulizi umezidi kuuongoza utafiti katika matumizi ya mbinu mwafaka za ukusanyaji data kutoka kwa watafitiwa walengwa.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Sura hii inadhihirisha mbinu ambazo mtafiti alizitumia wakati wa kukusanya data pamoja na wakati wa kufanya uchanganuzi. Matumizi hayo ya mbinu yalikuja kwa kuwa isingekuwa rahisi kwa mtafiti kuipata data kamili aliyoikusanya pasi na matumizi ya mbinu zenyewe. Isingekuwa rahisi kwa sababu data iliyopo vitabuni pekee isingelitosheleza bila kupata maoni mengine kutoka kwa wasomi na wataalamu wa sarufi ya Kiswahili. Halikadhalika, matumizi ya mbinu hizo yalirahisisha katika kupata data kutoka kwa watoa taarifa wa utafiti huu bila kusitasita hasa ilipozingatiwa kuwa mtafiti alikuwa ni mgeni wa mazingira ya utafiti ulikofanyika.

Kwa upande , mbinu hizo zilileta manufaa wakati wa uchanganuzi. Manufaa yenyewe yalikuja pale ambapo baadhi ya wakati na baadhi ya taarifa za wasailiwa au wahojiwa, zilipomletea usumbufu mtafiti katika kufahamika kwake. Ilimlazimu arudi tena kwa muhusika ili kupata ufafanuzi zaidi. Ifahamike kuwa sarufi ni taaluma ya sayansi inayozingatia misingi ya kisayansi Hivyo utafiti wa kisarufi huhitaji uwasilishaji wake uwe wa kisayansi vilevile. Hapa chini zimefafanuliwa mbinu ambazo mtafiti alizitumia mwanzoni mwa ukusanyaji data hadi hatima ya zoezi lilipofikia.

3.1 Eneo la utafiti

Utafiti huu ulifanyika visiwani Zanzibar katika Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharibi katika Mkoa wa Mjini na Magharibi, Zanzibar. Katika wilaya hizo, utafiti ulifanyika katika maktaba, vyuo vikuu na skuli za sekondari. Halikadhalika utafiti ulifanyika kwenye maskani za watu ili mtafiti apate kujitosheleza zaidi ya zile data za maktabani. Utafiti ulifanyika maskanini pia kwa sababu ya matumaini ya mtafiti kwamba kwahala huko pia wanaishi wataalamu ambao wana viwango vikubwa vya taaluma na hivyo ingekuwa rahisi kupata maoni yao yahusuyo matumizi ya kiambishi " h-" katika sarufi ya Kiswahili. Katika uteuzi huo wa eneo la utafiti, hapa chini zinawekwa sababu ambazo ndizo hasa zimetolewa kiini cha kufanyika kwa uteuzi huu.

Moja ilikuwa kupata urahisi na unafuu wa kila huduma ambayo mtafiti aliihitaji. Wepesi huo ulizingatia huduma za kitaaluma, huduma za akili na za mwili zikiwemo huduma ya chakula. Inafaa ifahamike kuwa hoteli na mikahawa salama mara nyingi huwepo katika maeneo ya mijini. Hivyo ilikuwa aula mtafiti huyu kufanyia utafiti wake kwenye eneo hilo kwa sababu ya Imani aliyokuwa nayo juu ya upatikanaji wa chakula bora, huduma njema pamoja na huduma

nyepesi ya usafiri. Jambo hilo la usafiri lilikuwa ni muhimu sana kwa sababu haikuwa vyema kwa mtafiti kutumia gari za umma ambazo mara nyingi zina shida ya ucheleweshaji. Usafiri pekee kwa mtafiti huyu aliye mgeni ulikuwa wa kukodi.

Katika eneo hilo ilitarajiwa kuwa wakazi wake mara nyingi walikuwa ni wenye kutumia lugha ya Kiswahili. Matarajio haya yalikuja kutokana na uzoefu tu wa mtafiti kwa kuona kuwa katika miji mingi wakazi wake huwa wanatumia lugha sanifu na pia lugha fasaha. Matumizi ya lugha hizo huwa ni muhimu kwa wageni kwa sababu huwa ni rahisi kufahamika kutokana na misamiati wanayoitumia pamoja na lafudhi ambayo huwa ni nyepesi na laini. Kwa sababu hiyo ndipo pia mtafiti alipoona haja ya kufanya utafiti wake kwenye eneo hilo ili kwake iwe ni rahisi kufanya mawasiliano na watoa taarifa wake.

Sababu nyingine ni pale alipobaini kuwa tawi la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania lipo kwenye eneo hilo. Kwake yeye alihisi kuwa hiyo ni fursa adhimu kwa 'mwanafunzi mtafiti' kufanya utafiti kwenye eneo la chuo anachosoma.

3.2 Watafitiwa

3.2.1 Walimu wa skuli za sekondari

Walimu wa sekondari wanajikita katika maarifa ya kina katika ufundishaji wa lugha. Na hivyo mara nyingi uchambuzi wa matumizi ya viambishi kadhaa vya kisarufi, wanao upeo mkubwa. Rai hiyo ilikuwa mwafaka kwa mtafiti na alifanya jitihada mno kuhakikisha kuwa kila skuli ambayo aliidhamiria aliiendea. Walimu wapatao 20 walitafitiwa kuhusu kiambishi cha "h-". Kigezo kilichozingatiwa kuteuwa walimu wa skuli za sekondari kilikuwa kufundisha Kiswahili. Pia waliteuliwa kwa idadi sawa kwa jinsi yaani 10 wa kiume na 10 wa kike.

3.2.2 Wahadhiri wa Vyuo Vikuu

Utafiti huu uliwahusisha wahadhiri wa vyuo viteule: wahadhari 10 wa vyuo teule hivi walishirikishwa. Vyuo ambavyo vilihusishwa na utafiti huu vilikuwa kama ifuatavyo:

9. Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) wahadhiri 3
Chuo Kikuu Huria (Tawi la Zanzibar) wahadhiri 3
Chuo cha Abdulrahman Al-Sumait
wahadhiri 2
Chuo cha Mwalimu Nyerere (Tawi la Zanzibar) Wahadhiri 2

3.2.3 Wataalamu wa sarufi

Utafiti ulifanyika katika Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) katika idara inayoshughulika na masuala ya sarufi na usahihi wa lugha ya Kiswahili. Idadi ya watafitiwa ilikuwa 10 (ikiwa ni pamoja na wataalamu wa kitengo cha kutunga kamusi)

3.2.4 Wazungumzaji wa kawaida wa Kiswahili

Utafiti ulihusisha wazungumzaji 10 wa kawaida wa Kiswahili ambao walitembelewa katika makazi yao. Data kutoka kwa watafatiwa zilikusanywa kwa njia ya hojaji na pia kwa maelezo yaliyotokana na mazungumzo ya kawaida hasa yaliyohusu dhana ya Uyakinishi na Ukanushi.

3.4 Mbinu za kukusanya data

3.4.1 Hojaji

Hojaji za aina mbili zilitayarishwa: moja kwa ajili ya wanafunzi na nyingine kwa ajili ya walimu wa shule za sekondari na wahadhiri wa Vyuo Vikuu.

Katika utafiti huu imetumika mbinu hii mojawapo ya ukusanyaji data. Ifahamike kuwa mbinu kwa kawaida hutumika ili imsaidie mtafiti kupata taarifa au data yake kwa urahisi. Kwa namna nyengine, mbinu hufasirika kama njia inayopasa kufuatwa wakati wa ukusanyaji data (Enon, 1998). Kwa kuwa ni njia, basi matumizi ya hojaji ni mojawapo ya njia muhimu katika ukusanyaji data. Hivyo basi, mbinu hii ilitumiwa na mtafiti pale ambapo ilishindikana kuwapata watoa taarifa kwa mahojiano ya ana kwa ana. Lakini pia, katika maeneo ya skuli na hata kwenye vyuo vikuu, ilitumiwa mbinu hii kwa dhamira mbili kubwa. Mosi, kupata kumbukumbu za kimaandishi, hasa ikizingatiwa kuwa taaluma ya sarufi kudhihirika kwake ni katika maandishi. Yaani, sarufi siyo taaluma ya kinadharia. Ni lazima ibainishwe kwa matendo. Mathalani ikiwa mojawapo ya aina za maneno ni nomino, basi ili mtu aweze kufahamu vyema ni sharti iwepo tungo ambayo ndani yake imo nomino. Halafu abainishiwe kuwa hiyo ndiyo nomino, na pengine abainishiwe kanuni za uandishi wa nomino na hubadilikaje kulingana na muktadha wa nomino hiyo.

Bila shaka mtafiti anapokusanya data kwa kugawa hojaji, hutumia muda mdogo zaidi kuipokea data hiyo hasa ikiwa watoa taarifa wapo mahala pamoja na ikiwa watajaza mahojaji kwa wakati kwa wakati mmoja. Haikataliki kuwa madhara mojawapo ya hojaji ni kuikosa kabisa au kuchelewa kwa muda mrefu katika upatikanaji wake kwa kuwa baadhi ya wanaopewa hufanya uzito katika kuyarudisha. Mara nyingi asilimia kubwa ya waliopewa, huwa wanazirudisha kwa wakati kukiwa na usimamizi mzuri.

Halikadhalika mbinu hii ilitumika kwa sababu walikuwapo baadhi ya watoa taarifa wasiokuwa tayari kufanya mahojiano kwa hofu au pengine hawakuwa fasaha katika uzungumzaji. Hivyo, watoa taarifa kama hao walipotambulikana ndipo walipopatiwa hojaji ili wajaze na kuandika maoni yao.

Vilevile, mbinu ya hojaji ilikuwa ni muhimu kwa mtafiti kwa sababu ilimsaidia kupata mawasiliano ya baadaye pale alipohitaji ufafanuzi wa ziada zama data ilipokuwa inachambuliwa. Tunasema hivi kwa sababu kwenye mahojaji hayo mlikuwa na sehemu ya utambulisho wa mtoa taarifa-wapi anaishi, kiwango cha elimu alichonacho pamoja na nambari yake ya simu. Mambo hayo yalikuwa ni muhimu kwa kuwa pale ilipotokea mtafiti kuhitaji ufafanuzi wa jambo zaidi, basi aliwasiliana tu na watoa taarifa wake. Hata hivyo isidhaniwe kuwa ilikuwa ni jambo la lazima kwa mtoa taarifa kuandika nambari yake ya simu yake. Kwa yule ambaye hakupenda kufanya hivyo, hiyari alikuwa nayo mwenyewe.

3.4.2 Mahojiano

Mbinu ya mahojiano ilianza kutumika wakati mtafiti akiwa anakusanya data maktabani. Mtafiti mara nyingi alikuwa na msaidizi ambaye alimsaidia maarifa. Maarifa hayo yalikuwa ni pamoja na kumfahamisha baadhi ya maeneo ambayo mtafiti alikuwa hajayafahamu. Hivyo mtafiti alihojiana na msaidizi wake hadi pale ufahamu kamili ulipopatikana. Mtafiti, kwa mfano, anakumbuka pale aliposoma kitabu fulani cha sarufi ambapo sehemu mojawapo iliyofafanua viambishi hakuielewa. Ndipo alipofanya mahojiano na msaidizi wake.

Mara nyingine mtafiti akifanya mahojiano na waendesha maktaba hususan pale ambapo alihitaji kazi fulani za sarufi. Kwa mfano, aliweza kufika maktaba na kufanya mahojiano na mkutubi ni namna gani tasnifu za sarufi zinavyoweza kupatikana kwa njia ya kuazima. Ndipo mahojiano yanapoanza kwa sababu mkutubi alikuwa hakubali kumuazima mtafiti kazi hiyo kutoka nje ya maktaba. Mtafiti alikuwa anahoji inakuaje vitabu viweze kupatikana hata viwe katika hesabu kubwa. Lakini tasnifu ishindikane hasa kwa mtu mgeni ambaye abadani hawezi kukimbia na tasnifu hizo kwa vile vielelezo vyake vya ruhusa ya kuingia nchini vipo. Kusema haki ilikuwa hapatiwi majibu sahihi zaidi ya kuambiwa kuwa ni marufuku kazi hizo kutoka nje. Kanuni ni nidhamu. Mkutubi hakuwa na kosa.

Kwa upande mwingine mbinu hiyo ilitumika wakati mtafiti alipokutana na watoa taarifa wengi. Kama ilivyoelezwa kabla kuwa utafiti huu pia ulifanyika makaazini, na hivyo mtafiti alikutana na watoataarifa hao kwa mahojiano. Sababu hasa ya kwenda makazini ilikuwa ni hofu ya mtafiti kukosa maelezo kamili ya matumizi ya kiambishi " h-" kwa asilimia mia moja. Mtafiti aliamini kwa kupitia wataalamu na wasomi hao bila shaka walikuwa na matumizi mengine. Maana, kupitia ndimi za wasomi na wanataaluma hao, yapo baadhi ya matumizi ambayo yalinukuliwa kutoka kwao ambayo kwenye vitabu hayamo. Hivyo mbinu hiyo ilisaidia mno katika upatikanaji wa data siyo za maktabani tu bali na zile za makazini pia.

Zaidi ya hayo, ifahamike kuwa utafiti huu ulichunguza mambo mengineyo kadhaa ambayo yalisaidia katika utambuzi na upatikanaji wa matumizi ya kiambishi " h-" kwenye tungo au sentensi za Kiswahili. Miongoni mwa mambo yaliyochunguzwa ni kama vile uzingatifu wa maumbo ya kiambishi " h-" pamoja na nafasi kiambishi hicho kinapojitokeza kwenye neno au maneno. Mambo hayo ya maumbo na nafasi zake yalikuwa muhimu kwa sababu yalileta manufaa katika hali zifuatazo.

Moja, yalimdhihirishia mtafiti kuwa kiambishi kanushaji cha Kiswahili siyo kimoja tu kama ambavyo baadhi ya watu hudhani. Lakini pia ilibainika kuwa mabadiliko ya maumbo kwa kiambishi " h" hutokea kulingana na mabadiliko ya nafsi. Na kwamba kama siyo uzingatifu wa mabadiliko ya nafsi, basi yasingepatikana maumbo anuwai ya kiambisi" h-".

Pili, katika utambuzi wa nafasi ya kiambishi " h-" ilibainika kuwa wanasarufi wangeweza kuunda kanuni za kisarufi ikiwamo ile kanuni

ioneshayo kwamba kiambishi " h-" kinapotumika kama kikanushi kwenye kitenzi kwamba ni sharti kikae mwanzo wa neno, nafasi ambayo imezoeleka kuwa ni ya nafsi pekee. Hivyo, mbinu hii ya mahojiano iliweza kumpatia tija mtafiti kwa kuibua mambo mengi ya kitaaluma yahusuyo taaluma ya sarufi.

3.4.3 Mbinu ya kuwa na Msaidizi Mtafiti

Ufanikishaji wa utafiti huu usingefikiwa kama siyo kwa msaada mkubwa wa mtafiti msaidizi. Huyo alimsaidia mtafiti katika majumuisho ya mambo kadhaa yafuatayo.

Kwanza alikuwa mfasiri wa lugha ya Kiarabu pale ambapo mtafiti ilishindikana kufahamika ipasavyo. Yaani, mara nyingi watoa taarifa walikuwa wanachanganya maneno. Na hivyo pale wanapochanganya maneno haikuwa rahisi kwa mtafiti kumfahamu mtoataarifa wake. Katika hali hiyo ndipo mtafiti alipoona haja ya kuwa na msaidizi wake ambaye ni mzawa, mwenyeji na anayeielewa lugha ya Kiarabu.

10. Pili, msaidizi huyo alimsaidia mtafiti katika suala zima la kufahamu kaida za utamaduni wa wenyeji. Kila jamii ina utamaduni wake. Mathalani baadhi ya watafitiwa hujali zaidi maamkizi ya kimila na kwamba ikiwa hukuwaamkia kwa maamkizi hayo huenda kile kilichokusudiwa kisipatikane. Ingawaje, mtafiti anakiri kuwa hayo hayakumpa taabu yoyote.

Tatu, msaidizi huyo alisaidia katika upatikanaji wa data kwa haraka sana. Ifahamike kuwa huyu msaidizi ni mzaliwa na mwenyeji. Popote alipoenda, alikubalika kiurahisi na hivyo aliitumia fursa hiyo kumtambulisha mgeni wake ambaye ni mtafiti. Jambo hilo katika maeneo mengi vitambulisho vya mtafiti. Havikudaiwa.

Nne, msaidizi huyo mara nyingine alimsaidia mtafiti katikia unukuzi wa baadhi ya kauli na kumfahamisha mtafiti usahihi wa baadhi ya tungo au sentensi.

Tano, mtafiti msaidizi alimsaidia mtafiti katika uratibu wa lugha iliyoandikiwa tasnifu hii pamoja na kumhariria. Mara nyingi mtafiti alishindwa kuweka vizuri mpangilio wa sentensi kulingana na kanuni za lugha ya Kiswahili, na hivyo, msaidizi alikuwa akiirekebisha.

Kwa jumla mtafiti msaidizi amekuwa mtu muhimu kwa mtafiti; kiasi kwamba kama angekosekana, huenda ukusanyaji data, uchambuzi na uwasilishaji huu usingekuwa maridadi kama hivi. Hivyo, mtafiti msaidizi, katika hali nzuri, ndiye aliyemsaidia mtafiti katika kuyabainisha matumizi ya kiambishi " h" cha sarufi ya Kiswahili.

3.4.4 Maandishi maktabani

Utafiti huu ulifanyika maktabani kwa kiwango kikubwa. Ililazimu kufanyika mahala hapo kwa sababu tangu mwanzo data za utafiti huu zilitarajiwa zipatikane maktabani. Uchunguzi wa matumizi ya kiambishi " h-" siyo rahisi kupatikana kwenye maeneo mengine ambayo ni kinyume cha maktabani. Huko kuna maandiko mengi ambayo yamebainisha baadhi ya matumizi hayo. Kwa mfano, kuna vitabu vya kila namna; kama vitabu vya sarufi, majarida ambayo ndani yake zimo makala zenye mwelekeo wa mada hii iliyotafitiwa na pia zilikuwamo tasnifu ambazo kwa namna fulani zimeeleza masuala ya viambishi kanushi, na kadhalika.

Katika ukusanyaji wa data maktabani, mtafiti alifika kwenye makabati maalumu ya kazi zinazohusika na kuanza kuchukua moja baada ya nyingine. Alitafuta sehemu akakaa kwa kujisomea ile hazina aliyonayo. Utaratibu ulikuwa kuangalia kwenye ‚yaliyomo' na baada ya kuona ukurasa unaozungumzia viambishi, au ukanushaji, ndipo alipokuwa anafungua kwa kudurusu. Pale alipopata habari inayohusiana na mada yake, alichukua kwa kuiandika kwenye buku maalumu au kwenye kompiyuta anayotembea nayo.

Halikadhalika huko maktaba, mtafiti pia aliingia kwenye intaneti kutafuta makala au tasnifu ambazo zimekuwa na uhusiano kwa mada yake. Nia ilikuwa ni kuzidi kujihakikishia kuwa mada aliyoitafiti haikuwahi kutafitiwa na mwenginewe. Kwa bahati tangu vitabuni, majaridani na kwenye tasnifu kadhaa wa kadhaa, pamoja na mtandaoni, hakuwahi kujitokeza mtafiti ambaye aliifanya kwa kina mada ya matumizi ya kiambishi " h-" katika sarufi ya Kiswahili.

Kwa jumla hapo maktabani mtafiti alikusanya data zilizojumuisha maana ya viambishi, aina za viambishi, maumbo malimbali ya viambishi, kazi za viambishi na mifano yake, pamoja na maumbo tafauti ya kiambishi " h-". Ukusanyaji huo uliendा sambamba na uchunguzaji wa matumizi kadhaa wa kadhaa ya kiambishi " h-" pamoja na kuchunguza mazingira ya kiambishi hicho kwenye maneno au/na sentensi. Jambo jengine ambalo mtafiti alilichunguza ni swala la umuhimu wa kiambishi " h-" hasa katika kuangalia umuhimu wa kuwapo kiambishi hicho kwenye maneno au sentensi na kinyume chake.

Baada ya ukusanyaji data wa maktabani kumalizika, mtafiti alifika kwenye maskani za watu na katika maeneo ya kazi kwa dhamira ya kufanya mahojiano na wataalamu wa sarufi. Pale alipokutana nao alifanya mahojiano nao yaliyokusudia kwanza, kupata taarifa ihusuyo maumbo ya kiambishi " h-" mengineyo ambayo ni kinyume na yale yaliyomo kwenye kazi za sarufi. Pili, ilikuwa ni kuulizia matumizi mengine zaidi ya kiambishi hicho. Pamoja na kupata maoni mengineyo yahusuyo kiambishi kinachotafitiwa. Kwa jumla yapo mapya ambayo yalipatikana kama Sura ya Nne ya utafiti huu ilivyobainisha.

3.5 Uchambuzi wa data

Taarifa kutokana na utafiti huu zililenga kujibu maswali ya utafiti yaliyotajwa katika Sura ya Kwanza (1.4). Taarifa hizo zimelinganishwa na kuwakilishwa kwa muhtasari katika majedwali ya takwimu na pia katika maelezo ya mtafitiwa pale ilipobidi, ili kuelewa data hizo kwa kina zaidi kuliko kielezeo chochote kinavyoweza kufanya.

3.6 Muhtasari

Sura hii imeonesha jinsi utafiti ulivyoandaliwa: mahali, watafitiwa, mbinu na vifaa muhimu. Baada ya maandalizi hayo utafiti ulifanyika. Matokeo ya maandalizi hayo data zilizopatikana zimewasilishwa katika Sura ifuatay

SURA YA NNE

UWASILISHAJI WA DATA, UCHAMBUZI NA MJADALA

4.0 Utangulizi

Katika sura hii data zimewasilishwa kulingana na aina za watafitiwa walioshirikishwa. Lengo la uwasilishwaji huu pamoja ucha uchambuzi nuzi ni kurejea katika maswali ya utafiti kama yalivyotolewa katika Sura ya Kwanza (1.4) Baada ya mawasilisho ya matokeo kwa kila swali la utafiti mjadala umefuatia kwa lengo la kutambua mambo yaliyosababisha matokeo hayo. Mwishoni mwa sura hii kuna muhtasari wa Sura nzima ambao umeeleza kwa kifupi, uchambuzi na mahitimisho yaliyofikiwa katika mijadala.

4.1 Taarifa za msingi za watafitiwa

Baada ya kutumia vigezo vya kuteua watafitiwa kama ilivyoelezwa katika Sura ya Tatu, utafiti huu ulihusisha jumla ya watafitiwa **50** kama ifuatavyo:

Wahadhiri (wa Vyuo Vikuu)	10
Wataalamu wa Sarufi (BAKIZA)	10
Walimu wa skuli (za sekondari)	20
Wazungumzaji wa kawaida (wa Kiswahili)	10
Jumla	**50**

Suala la kwanza katika uchambuzi wa data za watafitiwa lilikuwa kupata vigezo vya taarifa za jumla zinazohusiana na ujuzi na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Katika kipengele hiki makundi mawili yafuatayo yalibainishwa:

(i) Ujuzi wa Kiswahili wa jumla wa kwa watafitiwa na hasa ujuzi wa lahaja zaidi ya Kiswahili sanifu

(ii) Utumiaji wa taaluma ya lughawiya (isimu) katika shughuli za watafitiwa. Katika kundi hili vigezo vidogo vitatu vilizingatiwa ambavyo ni:

- Kiwango cha utambuaji wa kiambishi "h-" kama mofimu
- Mazingira ya kiambishi "h-" kinamotokea katika maneno ys Kiswahili
- Uamilifu (utumikaji) anuwai wa kiambishi "h-" katika lugha ya Kiswahili

4.1.1 Kiwango cha ujuzi wa Kiswahili

Kama ilivyotajwa hapo juu, kigezo hiki pamoja na kutaka kujua kiasi cha mtafitiwa kukijua Kiswahili (anazingatia kanuni zinazosimamia usahihi wa lugha na pia kukitumia Kiswahili katika miktadha mbalimbali kadiri ya mahitajio) kililenga iwapo anajua lahaja nyingine za Kiswahili mbali na Kiswahili sanifu. Hii ilisaidia kulinganisha na kutafautisha Kiswahili sanifu na lahaja nyingine hasa katika utmiaji wa kiambishi "h-". Matokeo ya utafiti kwa kuzingatia kigezo hicho yalikuwa kama yanavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 10: Ujuzi wa Kiswahili kwa viwango mbalimbali

Aina ya watafitiwa	Ujuzi bila taaluma	%	Ujuzi na taaluma	%	Zaidi ya lahaja moja	%
Wahadhiri	0	0	10	20	2	4
Wataalamu wa sarufi	0	0	10	20	4	8
Walimu wa skuli	0	0	20	40	2	4
Wazungumzaji wa kawaida	10	0	0	0	5	10
Jumla	10	20%	40	80%	13	26%

Katika **Jedwali 10** hapo juu imedhihirika kwamba watafitiwa walikuwa na viwango tafauti vya Kiswahili na pia ujuzi wa lahaja nyingine zaidi ya Kiswahili sanifu. Watafitiwa 10 (20%) walijua Kiswahili cha kawaida tu wala hawakuwa na taaluma yoyote juu sarufi yake. Jambo jingine muhimu lililojitokeza ni kwamba ni sifa ya kujua lahaja nyingine mbali ya Kiswahili sanifu. Watafitiwa 13 (26%) tu waliokuwa wana ujuzi wa lahaja nyingine. Hao ama walizaliwa nje ya mji wa Zanzibar au walijifunza lahaja nyingine mbali na Kiswahili sanifu kutoka kwa wazazi wao wenye asili ya lahaja hizo au walipata kufanya kazi kwingineko kabla ya mtafiti kukutana nao hapa Zanzibar. Waliobaki 37 (74%) walikuwa wazawa wa mji wa Zanzibar na wengi kati yao hawakuwahi kupata nafasi ya kujua lahaja nyingine.

4.1.2 Utumiaji wa taaluma ya lughawiya (isimu) katika shughuli za watafitiwa

Watafitiwa wote walijua Kiswahili lakini matokeo ya utafiti yamedhihirisha kwamba wanatofautiana katika utumiaji wa taaluma ya lughawiya (isimu) katika kukitumia Kiswahili katika shughuli zao kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 11: Uhitaji wa taaluma ya lughawiya (isimu) katika shughuli za watafitiwa

Aina ya watafitiwa	Wanaohitaji wa lughawiya (Isimu) daima	%	Wahitaji wa lughawiya (Isimu) mara chache	%	Wasiohitaji lughawiya (Isimu) kabisa	%
Wahadhiri	6	12	2	4	2	4
Wataalamu wa sarufi	10	20	0	20	0	20
Walimu wa skuli	6	12	2	16	2	4
Wazungumzaji wa kawaida	0	20	0	0	10	20
Jumla	22	64 %	4	8 %	14	28 %

Jedwali 11 la hapo juu limetuonesha uhitaji wa taaluma ya lughawiya (isimu) unatofautiana kati ya kundi moja na kundi jingine. Sura ya jumla ni kwamba idadi kubwa 22 (64%) inahitaji taaluma ya lughawiya (isimu) katika shughuli zao. Tukijumlisha watafitiwa wanaohitaji taaluma hiyo mara chache na ile isiyohitaji kabisa tunapata jumla ya watafitiwa 18 (36%). Uwiano huu ni mzuri kwa utafiti huu ambao kwa hakika unahitaji sana ujuzi wa taaluma ya lughawiya (isimu). Hata hivyo ni muhimu kutambua kwamba hata katika kundi kubwa la wahitaji wa lughawiya (isimu) kuna mambo yanayosababisha tofauti zinazojitokeza. Kwa mfano, katika makundi ya wahadhiri na walimu baadhi yao hawahitaji lughawiya (isimu) kabisa katika kazi zao ingawa kiwango cha ujuzi wao ni pamoja na utaalamu wa lugha walio nao hasa ikilinganishwa na wazungumzaji wa kawaida wasio na utaalamu na wala hawahitaji taaluma ya isimu katika shughuli zao. Wahadhiri 6 (12%) walisema wanahitaji lughawiya (isimu) daima lakini wahadhiri 2 (4%) hawahitaji lughawiya (isimu) kabisa kwa sababu walisema wao wanajihusisha zaidi na uwanja wa fasihi.

4.2 Kiambishi " h-" kama mofimu katika maneno ya Kiswahili

Kuweza kujua mofimu ni nini na kutambua umuhimu wake katika maneno ni suala linalohitaji ujuzi wa lughawiya (isimu). Kama tulivyojadili katika Sura ya Pili wanalughawiya (wanaisimu) wamefafanua mofimu kwa namna na mitazamo mbalimbali. Kwa jumla ni kwamba mofimu sharti ifanye kazi ya kisarufi k.m. wakati (njeo), ngeli, hsli ya uyakinifu, ukanushi, kategoria za maneno, n.k. mbali na kutambua kiambishi " h-" kama mofimu ilipasa watafitiwa pia waeleze japo kidogo. Watafitiwa walijibu swali hili kwa matokeo kama yanavyooneshwa katika Jedwali lifuatalo:

Jedwali 12: Utambuaji wa mofimu " h-" kama mofimu

Aina ya watafitiwa	Waliotambua mofimu “h-“ bila maelezo	%	Waliotambua mofimu “h-“ na kutoa maelezo	%	Walioshindwa kutambua mofimu “h-“	%
Wahadhiri	7	14	3	6	0	0
Wataalamu wa sarufi	0	0	10	20	0	0
Walimu wa skuli	8	16	12	24	0	0
Wazungumzaji wa kawaida	0	0	0	0	10	20
Jumla	15	30 %	25	50 %	10	20 %

Kwa mujibu wa **Jedwali 12** hapo juu inadhihirika kwamba jumla ya watafitiwa 15 (30%) waliweza kutambua angalau kiambishi " h-" kilikuwa mofimu. Sababu kubwa iliyotolewa ilikuwa ni kule kuweza kutofautisha maana ya neno kila ilipotokea ingawa hawakuweza kutoa maelezo yake. Jumla ya watafitiwa 15 (30%) walikuwa wahadhiri na walimu.

Wazungumzaji wa kawaida hawakuweza kabisa kujua jambo hili. Baadhi yao walishangaa na kusema

> Ati umesema…. simu, simo au shimo? Simu ndo nini? Sikupati vemea…hakika mbona sikuelewi! Hebu rejea tena tafadhali…

Watafitiwa waliotambua kiambishi " h-" na kutoa maelezo walikuwa 25 (50%). Kundi hili lilihusisha baadhi ya wahadhiri, wataalamu wa sarufi wote na idadi kubwa ya walimu wa skuli.

4.3 Mazingira ya kiambishi " h-" katika maneno ya Kiswahili

Kusudi la swali hili lilikuwa ni kujua iwapo mtafitiwa baada ya kutambua kiambishi " h-" kama mofimu angeweza kujua mahali katika neno kiambishi hicho kimetokea kama mofimu – yaani, iwapo kimetokea mwanzoni mwa neno au mwishoni mwa neno na kufanya kazi yake kama mofimu. Kwa mujibu wa majibu ya watafitiwa matokeo ya swali hili yamekuwa katika jedwali linalofuata:

Jedwali 13: Utofautishaji wa mazingira ya kiambishi " h-" katika maneno

Aina ya watafitiwa	Waliotambua bila maelezo	%	Waliotambua na kutoa maelezo	%	Walioshindwa kutambua	%
Wahadhiri	2	4	8	16	0	0
Wataalamu wa sarufi	0	0	10	20	0	0
Walimu wa skuli	5	10	15	30	0	0
Wazungumzaji wa kawaida	8	16	2	4	0	0
Jumla	14	30 %	36	70 %	0	0
Jumla	14	30%	36	70%	0	0

Jedwali 13 hapo juu limethibitisha kwamba hakuna aliyeshindwa kutambua tafauti ya nafasi kilimotokea kiambishi " h-" hata kama si wote walioweza kutoa maelezo ya kiambishi hicho kama mofimu. Jedwali linaonesha ya kwamba watafitiwa 36 (70%) waliweza kutafautisha mofimu hiyo. Hii kama ilivyokwisha kuelezwa kiambishi hicho kilisababisha kutokea kwa mabadiliko katika maana ya neno. Kinachoweza kusemwa hapa ni kwamba hata kama mtumiaji wa lugha hana taaluma ya lughawiya (isimu) lakini angeza kutambua kazi ya kiambishi kutokana na kuzingatia ujuzi alio nao unaomwongoza kujua usahihi wa neno au tungo kama asemavyo Chomsky katika kazi zake (1957 na 1965)

4.4 Uamilifu (utumikaji) anuwai wa kiambishi " h-" katika lugha ya Kiswahili

Lengo la swali hili lilikuwa kuona iwapo kiambishi kinao uhuru kiasi gani wa kiambishi " h-" kutokea katika lugha ya Kiswahili kinapokuwa kikifanya kazi ya kisarufi. Katika kukusanya data kuhusu suala hilo ilibidi kuona jinsi kiambishi "h-" kinavyoungana na irabu za Kiswahili (a, e, i, o na u) na kuwa ha-, he-, hi- ho- na hu- na kuunda maneno yanayokubaliwa katika Kiswahili. Matokeo ya utafiti juu ya swali hili yameoneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 14: Utambuaji wa uamilifu anuwai wa kiambishi " h-" katika lugha ya Kiswahili

Aina ya watafitiwa	Uamilifu wa kiambishi "h-" bila kutoa maelezo ya lughawiya (isimu)	%	Uamilifu wa kiambishi "h-" na kutoa maelezo ya lughawiya (isimu)	%	Kushindwa kutambua uamilifu wa kiambishi "h-"	%
Wahadhiri	2	4	8	16	0	0
Wataalamu wa sarufi	0	0	10	20	0	0
Walimu wa skuli	14	28	6	12	0	0
Wazungumzaji wa kawaida	8	16	0	0	2	4
Jumla	24	48%	24	48%	2	4%

Jedwali 14 hapo juu limeonesha kwamba idadi ya watafitiwa walioweza kutambua uamilifu anuwai wa kiambishi " h" bila kutoa maelezo ya lughawiya (isimu) ni sawa na ile idadi iliyotambua uamilifu huo na kutoa maelezo ya lughawiya (isimu). Hii ilitokana na kuchangia kiambishi " h-" katika dhana tofauti katika neno kama inavyobainika katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 15: Dhana anuwai za kiambishi " h-"

Dhana anuwai	Kiambishi " h-" kinachochangiwa
Hapa (mahali) hapo (mahali)	ha- (mahali)
Hiki (kioneshi) hicho (kioneshi)	hi- (kioneshi)
Hodi (umbo sahihi) hoi (umbo)	ho- (umbo kubalifu)
Hela (umbo) samehe (umbo)	he- (umbo kubalifu)
Ehe! (kushangaa) mheshimiwa (umbo)	he (umbo kubalifu)
Hujambo uhuru	hu- (nafsi na umbo kubalifu)
Haki msamaha	ha- (umbo)
Huamka asubuhi Jamhuri	Hu- (nafsi, mazoea na umbo)

Haishangazi kwamba watafitiwa wengi (96%) waliweza kutambua kwamba ingawa kiambishi " h-" kipo katika kila moja ya maneno hayo ambayo yanakubalika katika kiswahili lakini ni kama umbo tu katika maneno. Hata kwa wazungumzaji wa kawaida wa Kiswahili (16%) waliweza kuliona hilo. Uhuru wa kiambishi" h-" katika matumizi ni mkubwa (anuwai)

4.5 Muhtasari wa sura

Katika sura hii uchambuzi wa matokeo ya utafiti umefanywa. Mambo muhimu yaliyojitokeza ni kama yafuatayo:

i) Kwa watumiaji wa kawaida wa lugha ujuzi wa sarufi si jambo linaloweza kuelezeka kwa urahisi ingawa kanuni za sarufi huzingatiwa ili kuwaongoza katika usahihi wa lugha wanayotumia. Jambo hili ndilo linalowaongoza hata wanaotumia lugha katika shughuli zao mahususi kama tulivyowaona wahadhiri wa vyuo, wataalamu wa sarufi na walimu wa skuli.

ii) Pamoja na kuwapo kwa sarufi na taratibu zake, uhuru wa kutumia viambishi au maneno ya kategoria yoyote kama maumbo yanayokubalika katika lugha husika ni vigumu kuuwekea mpaka.

iii) Kazi kubwa ya kiambishi "hu-" ni ya kisarufi (mofimu) lakini kama mofimu huweza kubadilika katika umbo jingine bila kuathiri maana inayo kusudiwa k.m. kiambishi hu- cha ukanushi huweza kuchukua umbo la si- katika Nafsi ya Kwanza (Umoja) bila kuathiri dhana ya kukanusha kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo:

Jedwali 16: Viambishi vya Ukanushi katika nafsi (Umoja)

Nafsi katika Umoja	Kiambishi cha Ukanushi
Mimi siandiki	**si-**
Wewe huandiki	**h-**
Yeye haandiki	**ha-**

SURA YA TANO

MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Sura hii imewasilisha vipengele vitatu muhimu ambavyo ni muhtasari wa kazi, hitimisho la utafiti na mapendekezo ya utafiti huu. Katika muhtasari kumeelezwa kwa ufupi kabisa maelezo ya kila sura. Yamewekwa bayana masuala muhimu yanayoongelewa kwenye sura ziinazohusika. Aidha ni muhtasari huo unaonesha namna kila sura ilivyo na mshikamano na sura iliyoifuata.

Kwa upande wa hitimisho, ni kwamba kipengele hiki kimeeleza kwa ufupi matokeo ya kazi yote pamoja na kubainisha umuhimu wa kila sura na namna sura hizo zilivyoweza kushikana hadi kukamilika kwa kazi hii.

Kipengele cha tatu cha mapendekezo kimewasilisha mapendekezo ya mtafiti. Pindipo wahusika wangekuwa wasomi au jamii na Serikali, wangeamua kuyafanyia kazi, Sarufi ya Kiswahili ingepiga hatua zaidi. Mapendekezo yanadokeza wazi kuwa hapana anayeweza kuiendeleza, kuimarisha, kuitetea pamoja na kuitatulia sarufi matatizo yake, isipokuwa wanataaluma wa sarufi wenyewe.

5.1 Muhtasari wa utafiti

Katika Sura ya Kwanza ya utafiti huu vipengele kadhaa vya msingi vimeangaziwa. Vipengele vilivyomo ni usuli wa utafiti ambao umebainisha chanzo cha kufanyika utafiti huu. Kuna suala la utafiti ambalo limeonesha sababu ya utafiti kufanyika. Halikadhalika, yapo madhumuni ya utafiti - makuu na mahususi. Hayo ndiyo dira iliyobainisha makusudio ya utafiti huu. Vilevile mna madhumuni ya utafiti ambayo yamekamilishwa na maswali ya utafiti ambayo ndiyo yaliyosaidia kupatikana kwa data zilizokusanywa. Kwenye sura hii pia mumeongelewa mawanda ya utafiti ambayo yameweka wazi kuwa licha ya viambishi aina kwa aina kuwapo, lakini utafiti umejikita kwenye matumizi ya kiambishi " h-" pekee. Sura imemalizia na kutaja umuhimu wa utafiti pamoja na ukomo wa kazi hiyo. Mambo muhimu yaliyochunguzwa katika ukomo wa kazi hii ni pamoja na kutambua kwamba utafiti huu umefanywa katika eneo dogo tu la Zanzibar na kwa watafitwa wachache tu. Si kiwakilishi halisi kuhusu sarufi nzima ya Kiswahili au jamii nzima ya watumiaji wa Kiswahili.

Sura ya Pili usomaji makini wa kazi tangulizi, hasa za maandiko. Hapa, maandiko mengi ya sarufi ya Kiswahili yalichunguzwa. Baadhi yalihusu nadharia na mikabala iliyosomwa na kuchunguzwa iwapo yalikuwa na mnasaba na mada hii. Usomaji huo siyo tu ulimsukuma mtafiti kufanya utafiti huu bali pia ulikuwa mwongozo kwa baadhi ya hatua za utafiti. Mambo yaliyoangaziwa ni kama vile, utambuaji wa aina za viambishi, kutaja baadhi ya kazi za viambishi pamoja na kurahisisha matumizi bora ya mbinu za utafiti. Halikadhalika, kwenye sura hii, Nadharia ya Uamilifu (Utumikaji) pamoja na Mkabala wa Uchunguzi Tofautishi zilielezwa na jinsi zilivyo msingi mkuu unaosaidia kupatanisha taaluma ya lughawaya (isimu) kwa upande mmoja na matumizi halisi ya watumiaji wa Kiswahili kwa upande wa pili.

Katika Sura ya Tatu mbinu za kukusanya data ziliwasilishwa pamoja na zana zilizotumika katika kukusanya data. Kwa mfano, imetajwa sababu ya kuwa na Mtafiti Msaidizi ambaye alikuwa kiungo muhimu sana katika kufanikisha utafiti tangu kukusanya data zilizokusudiwa na kwa kiwango kilichohitajika. Wakati mwingine watafitiwa walipokuwa wakifanya mahojiano, ililazimu Mtafiti Msaidizi amfahamishe mtafiti kile kilichokuwa kikiendelea kwa sababu uzungumzaji wa wenyeji/wazawa wa Kiswahili, ulikuwa mgumu kiasi kwa mtafiti ambaye si mzawa wa lugha ya Kiswahili.

Sura imeendelea kwa kuonesha mfuatano wa matokeo ambao ni kuwapo kwa jumuiya, kufanyika uteuzu na kueleza eneo la utafiti, kutaja vifaa vya utafiti vilivyotumika, uteuzi wa watafitiwa pamoja na kueleza kwa muhtasari namna data zilivyokusanywa na kufanyiwa uchambuzi.

Sura ya Nne ndiyo kiini cha kufanyika utafiti. Hapa ndipo data zilipochambuliwa hatua kwa hatua. Data zenyewe zimechambuliwa kwa mikabala yote ya miwili ya takwimi na kuwasilishwa katika majedwali na pia mbinu ya maelezo kwa kukariri waliyosemwa hasa na watafitiwa ili kupata undani wa taarifa zilizotolewa. Mbinu zote zilikuwa muhimu na zilitegemeana sana.

Katika sura hii, mtafiti alirejelea maswali ya msingi ya uchunguzi na kuchambua matokeo yake. Uchambuzi ulianza na taarifa za msingi za watafitiwa binafsi kuhusu ujuzi wao wa lugha na uwezo wa kutumia taaluma ya lughawiya (Isimu) katika uchambuzi wa kiambishi " h-" za wahojiwa. Wahojiwa walioteuliwa walikuwa ni wa viwango tofauti vya ujuzi wa Kiswahili na jinsi walivyokitumia katika shughuli zao.

Baadaye, ukafuata uchambuzi wa maswali ya utafiti; mafupi na marefu, ambayo kimsingi ndiyo yaliyotumika kwenye ukusanyaji data. Majibu ya maswali hayo ndiyo yaliyomwezesha mtafiti kufanya uchambuzi wa data hiyo na kujua fasili ya data hizo kuhusiana na watumiaji wa lugha wa hali mbalimbali – wenye taaluma ya lughawiya (isimu) ya Kiswahili na wale wasio nayo.

Sura ya Tano ni sura iliyobeba mambo matatu muhimu – muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

5.2 Hitimisho la utafiti

Kwa ufupi kabisa utafiti huu ulifanyika kwa nia ya kuchunguza matumizi ya kiambishi " h-". Kabla ya hapo ilidhaniwa kwamba kiambishi hiki kina dhima ya kuwa mofimu ya ukanushi zaida. Ilidhaniwa kukosekana kwa kiambishi hicho huenda ukanushi wa Kiswahili nao ungekosekana. Mnasaba huo umebainisha kuwa kiambishi hiki ni kiambishi muhimu na chenye uzito uliyo mkubwa. Haidhuru viambishi vilivyobaki pia vina uzito wa hali ya juu, lakini kiambishi " h-" kinapewa kipaumbele zaidi.

Bila shaka, utafiti umekuwa na faida kwa kuwa yapo pia matumizi mengine ya kiambishi " h-" yaliyobainika. Halikadhalika, faida nyingine kwamba kupitia uchambuzi wa Sura ya Nne na ufafanuzi wa Sura nyinginezo, taarifa muhimu zimeweza kupatikana. Ndiyo maana kwenye ripoti hii; hasa katika Sura ya Nne, mna taaluma aipatayo msomaji kuhusu maana ya baadhi ya dhana, aina ya baadhi ya vipashio au vijenzi, pamoja na ufafanuzi wa matokeo ya aina nyingi.

11. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Uamilifu (Utumikaji) ambayo husisitiza kuwa kila kitu/kiungo kina utendakazi wake hapo kilipo. Matumizi ya nadharia hii yalisaidia katika kutoa dira kuwa kiambishi " h-" kwa kuwa ni kiungo katika aina nyingi za maneno, hasa kwenye vitenzi, kinao pia uamilifu mwingi kama kipashio katika lugha ya Kiswahili. Ndipo kilipotafitiwa na kuthibitishwa kuwa kiambishi hicho siyo kuwa hutumika kwa ukanushi tu bali pia hutumika kwenye matumizi mengine ya kisarufi. Vilevile, Nadharia ya Uamilifu (utumikaji) ilimsaidia mtafiti kwenye uundaji wa madhumuni.

ya utafiti na katika maswali ya utafiti wenyewe ambayo yameambatanishwa kama viambatanisho katika tasnifu hii. Ilivyo hasa, madhumuni mahsusi yote yalikumbatia moja kwa moja nadharia hiyo. Yakirejelewa madhumuni ya la pili na ya tatu ya utafiti huu, yameonekana wazi namna yanavyorandana na Nadharia ya Uamilifu (Utumikaji). Hapa yanaorodheshwa madhumuni hayo kusudi yawe ni ukumbusho na pia yaweze kuonekana kwa namna yalivyo na mshikamano na nadharia iliyotajwa.

i) Kubaini umbo la kiambishi " h-" katika maneno
ii) Kubainisha nafasi ya kiambishi " h-" katika maneno
iii) Kutambulisha uamilifu wa aina mbalimbali wa kiambishi " h-" katika maneno

Kutokana na maswali hayo, utafiti umeweza kugundua mambo yafuatayo kuhusu matumizi ya kiambishi " h-" kati ya watafitiwa:

i. Utafiti umegundua baadhi ya wasomi wa sarufi hawakuwa na muda wa kutoa ufafanuzi wa yale waliyoulizwa.
ii. Utafiti umegundua kuwa maandiko ya sarufi ni machache. Hayo yaliyopo yana mivutano ya kimawazo kiasi kwamba mara nyingine msomaji huwa hajui ashike wapi. Hii ni kwa sababu kuna aina tofauti za maneno na ndani ya kila aina kuna viwango tofauti.
iii. Utafiti umegundua kuwa watafiti wengi hupenda kutafiti fasihi kuliko sarufi. Mtu aendapo maktaba si haba akute kila penye kazi takribani 8, saba ni za fasihi na moja tu ndiyo inayohusu sarufi au isimu. Yawezekana sarufi huhitaji makini zaidi katika kuchambua kanuni zinazohifadhi usahihi na ukubalifu wa lugha kuliko matumizi ya maelezo kama fasihi ifanyavyo.

5.3 Mapendekezo

Baada ya utafiti huu mapendekezo yafuatayo yanatolewa:

i) Utafiti ufanywe katika eneo pana zaidi na hasa katika lahaja za Kiswahili. Kazi kama hizo zitatoa mwanga zaidi kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili ambayo ni pana na inayoendelea kuenea mahali pengi katika Bara la Afrika na nje ya bara hili.
ii) Utafiti wenye kuongeza taaluma ya lughawiya (isimu) utiliwe mkazo ili kugundua utajiri ulio katika lugha ya Kiswahili na hata katika lugha nyingine.
iii) Taaluma ni jambo linalokamilishwa na ujuzi wa watumiaji wa kawaida wa lugha. Watumiaji hao ndio kisima ambamo taaluma itachota hazina ya vito vilivyomo katika lugha na hivyo watafitiwa hao wasipuuzwe.

Ufanyike uchunguzi wa maumbo ya kiambishi " h-" ili yapatikane matokeo ya swali hili kama ifuatavyo:

i. Kiambishi" h-" kina maumbo mawili. Umbo moja ni maalumu kwa matumizi ya nafsi ya kwanza tu (umoja). Kwamba, mtumiaji anapokanusha, nafsi ikawa ni ya kwanza (umoja), hawezi kutumia kiambishi" " h-". Kiambishi kanushi ambacho itampasa akitumie ni /si-/. Mfano,

a. **Si**kuja tena
b. **Si**tolalamika abadan
c. **Si**jasema kitu

ii. Nafsi nyingine zilizobaki huwakilishwa na kiambishi halisi chenyewe " h-". Kwa mfano,

a. **H**atutamani Maisha (nafsi ya 1, wingi)
b. **H**uaminiki katu (nafsi ya 2, umoja)
c. **H**ammwelezi lolote (nafsi ya 2, wingi)
d. **H**asikizi la mzazi (nafsi ya 3, umoja)
e. **H**awakutoa mchango (nafsi ya 3, wingi)

Madhumuni ya pili yalimtaka mtafiti achunguze nafasi ya kiambishi " h-" katika maneno ili hatimaye aweze kukibainisha. Ugunduzi uliofanyika ni kwamba kiambishi " h-" kina nafasi mbili hadi tatu kwenye maneno. Nafasi moja hujitokeza pale ambapo kiambishi hicho hutenda kazi ya ukanushi na kwamba, daima nafasi yake huwepo mwanzoni mwa neno. Yaani, kwenye ukanushi, kiambishi " h-" ni shurti kivitangulie viambishi vilivyobaki kwenye neno/maneno. Kwenye hali hii, kiambishi " h-" hurahisisha kueleweka kwa kazi ya kisarufi ya kiambishi hicho

Nafasi ya pili hukaa pia mwanzoni mwa neno pindipo kiambishi hicho kitakuwa na uamilifu wa kusaidia katika uundaji wa neno. Wakati kiambishi " h-" kipo hapo, utenda kazi wake huonekana katika hali iliyo fiche. Matumizi yake huwa yamejificha. Wala huwa haiwi rahisi kwa mtumiaji kuweza kubaini uamilifu (utumikaji) wake hadi itokeapo kudondoshwa na kuwekwa kiambishi kingine ndipo matumizi yake yatakapotambulikana kwa sababu kiambishi hicho kingine, husababisha neno hilo kuwa na maana nyengine. Kwa mfano,

a. **h**ama – **h**amia –**h**amisha

Kwenye mfano huo, kiambishi" h-" kikidondoshwa na kuwekwa mbadala wake kama vile kiambishi " z-", neno hilo sasa litabadilika umbo na kuwa hivi:

b. **z**ama – **z**amia – **z**amisha

Kwa kuwekewa kiambishi "z-/" maana na maumbo ya maneno yote yamebadilika katika mfano (b)

Wakati mwengine kiambishi "h-" huwemo katikati ya mzizi wa neno kama vile,

a. ru**h**usa
b. sta**h**iki

lengo la tatu lilikuwa ni kutambulisha uamilifu wa kiambishi " h-" katika maneno. Lengo hilo pia lilifikiwa vyema. Matumizi ya kiambishi hiki yalidhihirika. Mfano,

i. Kutenda ukanushi
ii. Kuonesha ukaribu na umbali
iii. Kusaidia kuunda mzizi wa neno
iv. Kusaidia katika maamkizi

v. Kuchukua nafasi ya nafsi
vi. Kuunganisha nafsi zote
vii. Kuonesha matumizi ya ngeli
viii. Kusimama nafasi ya wakati (njeo)

Baada ya utafiti kumalizika imegundulika kuwa kiambishi " h-" kina matumizi yaliyotajwa hapo juu. Hivyo, ni wajibu wa wanataaluma, na hasa waandishi wa vitabu wasisalie kwenye kazi moja au mbili tu ya kiambishi hiki, bali waende zaidi mbele ili wanafunzi wetu na wasomi wa sarufi kwa jumla waweze kupata utambuzi huo.

5.4 Mapendekezo ya utafiti

Utafiti unayo mapendekezo yafuatayo,

i. Jamii ihamasishwe kujiunga na programu za sarufi ya lugha ili ziweze kufanya utafiti mbalimbali wa lughawiya (isimu). Kama suala hili halitazingatiwa ipasavyo, taaluma ya sarufi itapata udhaifu na hatimaye kukosa watetezi.
ii. Wanafunzi tangu kwenye ngazi za msingi, wazoweshwe na kushajiishwa kuipenda sarufi. Ili hapo watapofikia katika ngazi kubwa za kitaaluma, iwe rahisi kwao kusoma sarufi.
iii. Kufanya utafiti ni gharama. Taasisi na mashirika ni vyema kuungana na watafiti pale wanapopeleka maombi yao ili kuwapunguzia mzigo. Tija ya utafiti wao siyo tu kwa wao lakini pia ni kwa Taifa.
iv. Utafiti unaofanyika, baada ya kumalizika na kupitishwa rasmi, ni vyema kuwe na mfuko maalumu ambao utatumika katika uelimishaji umma wa matokeo ya utafiti huo.
v. Ikiwezekana, wanasarufi wawe na jumuiya yao ambayo itawaunganisha kuwa pamoja na kufanya mijadala kadhaa wa kadhaa ihusuyo sarufi ya Kiswahili.

MAREJELEO

Alzarouk, J (2010) Matatizo yanayowapata Wanafunzi Walibya Katika Kujifunza Viambishi vya Njeo Katika Lugha ya Kiswahili. Tasnifu ya M.A. (Kiswahili), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Dar es Salaam (Haijachapishwa)

Ali, S. (2015) Tofauti za Msamiati Baina ya Kiswahili cha Chake Chake na Kiswahili cha Micheweni Katika Kisiwa cha Pemba. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam. (Haijachapishwa)

Batibo, H. (2010) Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili Dar essalaam TUKI

Habwe, J. & Karanja, P (2004) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*, Nairobi: Phonix Publishers Ltd

Khamis, A. (2011) Uchambuzi wa Kiswahili Fasaha: Sarufi na Lughawiya Zanzibar Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani

Kihampa, M. (2003) *Sarufi ya Kiswahili: Shule za Msingi.* Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers

Kihore, Y., Massamba, D.P.B., Msanjilla, Y.P. (2012) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA):Shule za Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI

Kindly, N. (1986) *Matumizi ya Sarufi.* Dar es Salaam: Printpak (T) Ltd

Masebo, J. & Nyangwine (2002). *Kiswahili Kidato cha 3 na 4.* Dar es Salaam: Afroplus Industries Ltd.

Mdee, J. (1996) *Sarufi ya Kiswahili: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: DUP Ltd

Mkude, D. (2010) *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili* (uk. 47) Dar es Salaam: TUKI

Mgullu, R. (2010) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi Longhorn Publishers (K) Ltd

Msanjila, Y. P. (1985) Tafauti za Msingi Kati ya Tungo Nomino na Tungo Vitenzi katika Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI

Mohammed Taher (2013) Tofauti ya Viambishi Kanushi Kati ya Kiswahili na Kiarabu. (Tasnifu ya M.A. (Kiswahili) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Dar es Salaam (Haijachapishwa)

Rubanza, Y. (2003) *Sarufi: Mtazamo wa Kimuundo.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Dar es Salaam